## KESI MAGUNIA MKAA
‘Viatu chakavu vilitumika katika kuchoma mwili mke aliyeuawa’



UKURASA 7

## BOSI auawa kisa Sh. 800,000/- za mauzo nguruwe

UKURASA 3




UKURASA 11


# Nipashe

Jumamosi Julai 1, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581358

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US




Kamanda wa Polisi Mkoa wa Simiyu, ACP Edith Swebe

### UTATA KIFO MWOSHA MAGARI

# Mama adai mwanawe aliuawa na polisi wawili

**POLISI** wadaiwa kutoa rambirambi 200,000/-, kulipia jeneza, gharama za mochwari...*Endelea ukurasa wa 2*

# Kumekucha miradi mipya mabasi yaendayo haraka

UKURASA 4



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi na Mkewe Mama Mariam Mwinyi, wakitembelea moja ya banda la maonyesho la Kampuni ya China, baada ya ufunguzi wa Mkutano wa Tatu wa Ushirikiano wa Biashara kati ya China na Afrika katika Jimbo la Hunan, nchini China. **PICHA: IKULU**

UKURASA WA 9

### SERA, MITAALA MIPYA ELIMU:
## JK ATAKA UBORA WAHITIMU UMULIKWE

RAIS mstaafu Jakaya Kikwete, maarufu JK, ameshauri katika mabadiliko ya Sera ya Elimu na mitaala, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia itilie mkazo suala la ubora ili kukidhi mahitaji ya soko...

## Watumishi wabainika kuchomoa nyaraka, kuuza ardhi kinyemela

UKURASA 2

**MICHEZO** KOCHA YANGA APANGUA RATIBA MAANDALIZI UK. 24

**KATUNI** UK. 6

## Waziri abaini watumishi kuchomoa nyaraka na kuuza ardhi kinyemela

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula, amebaini kuwapo na watumishi wa Jiji la Dodoma wanaochomoa nyaraka za wananchi za masuala ya ardhi na kuchangia migogoro ya ardhi jijini hapa.

Hatua hiyo inakuja zikiwa ni siku chache baada ya Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kubainisha kutoridhishwa na utatuzi wa migogoro ya ardhi katika jiji hilo.

Waziri Mabula alibainisha hayo jana baada ya kukutana na wananchi wa jiji hilo ikiwa ni hatua mahsusi ya kushughulikia migogoro hiyo na mkwamo wa upatikanaji wa hatimiliki za ardhi.

Alitoa kauli hiyo baada ya mwananchi Shemaya Bihopho kueleza kuchelewa kupewa hati, hali iliyosababisha kiwanja chake kimoja kupewa mtu mwingine ambaye ameshapewa hati. "Nina taarifa za kina za watumishi wa jiji ambao wanachomoa nyaraka za wananchi, wanaweka nyaraka zingine na kurudisha tarehe nyuma na baadaye kuuza kiwanja kwa watu wengine," alisema. Waziri Mabula alisema mtumishi atakayebainika kuwakamishwa wananchi, atashughulikiwa na kutoa rai kwa wananchi kuwa makini na vishoka wa ardhi.

Alimwagiza Mkurugenzi wa Jiji John Kayombo kufuatilia kwa kina kiwanja ambacho Ofisa wa Jiji aliagiza umiliki uende kwa mtu mwingine wakati yupo anayedai ni chake.

Kiongozi huyo alibainisha tatizo la ardhi jijini humo linajumuisha mgogoro wa fidia za kiwanja, upimaji shirikishi ambao haukufanywa vizuri, kumilikishwa zaidi ya mara mbili, kutotekeleza ahadi ya kutatua migogoro na uelewa duni wa wananchi.

Alisema serikali iliwaondoa vibarua zaidi ya 120 ambao walikuwa hawapokei mshahara, hawalipwi posho na hawana mikataba lakini ni mabosi katika Jiji la Dodoma katika ofisi ya halmashauri.

"Ninakuagiza Mkurugenzi wa Jiji kuhakikisha ajira zote za mkataba zinafuata sheria na kuhakikisha wanawafanyia usahili pamoja na kuwaondoa. Juzi tulimkamata mwingine yuko site (eneo la kazi).

"Nitoe rai kwa wananchi ukikutana na mtu mtaani na unajua huyu ni kibarua na kama huna uhakika kama ni kibarua, mwombe akuoneshe kitambulisho, bado wako wengine mitaani,"alisema.

Pamoja na hayo, alisisitiza wananchi kufuata sheria na taratibu zilizowekwa katika ujenzi na kusisitiza Dodoma haitakiwi kuwa na ujenzi holela. "Hatutaki kuona kila kona kuna fremu za maduka, nitoe rai kwa wana Dodoma hatuhitaji ujenzi holela. Kwa sasa kuna watu watakuwa wanapita mitaani ukikutwa unajenga bila utaratibu nyumba yako itabomolewa," alisema.

Mkurugenzi wa Jiji hilo alisema mpaka sasa kuna viwanja 3,995 ambavyo wananchi wanapaswa kufidiwa na kuwa mkakati ulipo ni kuwa watatumia viwanja 1,037 vilivyopimwa Nala.

Pia alisema kwa wale watakaokuwa hawajafidiwa, halmashauri ina mpango wa kupima viwanja 6,000 na sehemu ya viwanja hivyo vitatumika kufidia viwanja 2,958 na kumhakikishia waziri kuwa tatizo hilo litaisha ndani ya mwaka wa fedha wa 2023/24.



Mhifadhi maeneo Tengefu ya Dar es Salaam, Pangu Iswalala (kushoto), akionyesha mitumbwi iliyokuwa ikitumika kwenye uvuvi haramu, katika ufukwe wa bahari ya Hindi, eneo la Kivukoni, jijini humo jana, baada ya kukamatwa na polisi wanamaji. Wengine ni Meneja wa Marine Park, Immaculate Semesi (wa pili kushoto) na Kamanda wa Kikosi cha Polisi Wanamaji, ACP Moshi Sokoro. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Adai mwanawe kuuawa na polisi

**Na Alex Sayi, MASWA**

ANNA Manyuru (70), mkazi wa Mtaa wa Zambia, Kata ya Malampaka wilayani Maswa mkoani Simiyu, ambaye ni mama mzazi wa Mandela Petro (26), amedaia mwanawe huyo aliuawa kwa kushushiwa kipigo na askari wawili wa Jeshi la Polisi mkoani humo wakimtuhumu kuiba betri ya sola.

Familia ya marehemu pia imedai kuwa baada ya kijana huyo kuuawa kikatili, ilipatiwa rambirambi ya Sh. 200,000 na jeshi hilo.

Mwandishi alipomtafuta Kamanda wa Polisi Mkoa wa Simiyu, Edith Swebe, kutolea ufafanuzi wa tukio hilo, alisema hawezi kuzungumzia kwa madai kuwa ngazi za juu zimeunda timu ya kufanya uchunguzi wa suala hilo.

Katika mazungumzo na Nipashe nyumbani kwake juzi, mama huyo alidai kuwa Juni 11, mwaka huu, askari polisi wawili aliowataja kwa jina moja mojal Afande Gaspar na Afande Jofu, walimkuta kijana wake mtaani na kumshushia kichapo kilichosababisha umauti wake wakimtuhumu kuiba betri la sola.

"Nina watoto watatu pekee na huyu ndiye alikuwa wa mwisho niliyekuwa ninamtegemea kutokana na baba yao kuzeeka lakini bila huruma wamempiga, baada ya kuzidiwa wakampelekea kusikojulikana," alidai mama huyo.

Alidai kuwa baada ya tukio hilo, aliamua kwenda kituo cha polisi kumwona mwanawe na alipowasili, aliambiwa kuwa 'umechelewa, muda wa chai umeisha, rudi wakati wa chakula'.

Anna alidai kuwa katika udadisi wake, alibaini kuwa muda huo mwanawe alikuwa njiani kupelekwa hospitalini kutibiwa.

"Baada ya kujua kuwa anapelekwa hospitalini, ikanibidi niende huko ambako pia walinizuia kumwona, kumbe alikuwa tayari ameshafariki dunia," alidai.

Lugo Petro, kaka wa marehemu, alidai mbele ya mwandishi kuwa baada ya tukio hilo, walipewa taarifa kuwa ndugu yao alipigwa na wananchi wenye hasira kali, wakimtuhumu kuiba baiskeli kisha kupelewa hospitalini ambako alipatwa na umauti.

"Walipofika msibani, tuliwauliza, hawakuwa na majibu lakini cha kushangaza waligharamia mazishi na kutoa fedha za rambirambi Sh. 200,000/- huku wakidai kutokuhusika na kifo cha ndugu yetu," alidai.

Mwandishi alipohoji kinachodaiwa kugharamiwa na polisi msibani, Petro alidai "walilipia jeneza, gharama za mochwari na msibani wakaleta lita 20 za mafuta, kilo 50 za maharagwe, kilo 150 za mchele na unga wa ngano. vitu hivyo walimpatia mfanyabiashara Kija Swani ili avilete msibani."

Mwandishi pia alizungumza na Mwenyekiti wa Mtaa wa Zambia linakodaiwa kutokea tukio hilo, Tungu Masolwa, alikana kuwapo tukio la wizi wa baiskeli wala mtu yeyote kupigwa au kuuawa na wananchi wenye hasira kali.

Baadhi ya wakazi wa mtaa huo, ambao baadhi waliomba hifadhi ya majina yao, walidai taarifa za kijana huyo kupigwa na wananchi si za ukweli. Wanachokijua, alikamatwa na polisi wakati anakunywa pombe katika Baa ya Mayunga, wakimtuhumu kuiba betri la sola.

"Tulikuwa tunafanya naye kazi hapa kijiweni akituoshea pikipiki, magari. Pia alikuwa fundi rangi. Ni kweli alikuwa anatuhumiwa kufanya matukio ya wizi lakini hakupigwa wala kukamatwa na wananchi," alidai mmoja wa mashuhuda hao.

Mzee Nyungu Athumani, mkazi wa Malampaka, alidai matukio ya askari polisi kutumia nguvu kupita kiasi yamekuwa yakijirudia katika kituo tajwa.

Alidai kuwa miaka miwili iliyopita, askari wa kituo hicho walidaiwa kupiga mtu hadi kuzimia, hali iliyosababisha wananchi kukishambulia kituo na kufanya uharibifu.

"Tunashindwa kuelewa hiki kituo kina shida gani. Ni miaka miwili tu imepita walipiga mtu akazimia, wananchi wakabomoa kituo. Leo tena wamepiga hadi wameua. Washukuru tu kwa kuwa wazee tulikaa tukawasihi wananchi wasifanye uharibifu tena kama miaka ya nyuma, lakini yule kijana (aliyefariki dunia) walimpiga hadi kuzidiwa kisha wakaondoka naye," alidai Mzee Athumani.

Diwani wa Kata hiyo, Renatus Mashara, alimwambia mwandishi kuwa hana taarifa zozote zinazoonyesha kuwa kijana Mandela alipigwa na wananchi kwa tuhuma za wizi wa baiskeli.

"Ukweli ni kuwa marehemu alikuwa anatuhumiwa kuwa na tabia ya wizi wa mara kwa mara na alikuwa anatumikia kifungo cha nje cha mwaka mmoja lakini hajauawa na wananchi kwani hatuna tukio hilo katika kata hii," alisema.

Kufuatia kauli ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Simiyu, Edith, kuwa suala hilo linafanyiwa kazi ngazi za juu, mwandishi alimtafuta Msemaji wa Jeshi la Polisi, David Misime, ambaye aliahidi kutoa ufafanuzi baadaye.

"Nitazungumza naye (Kamanda wa Polisi Mkoa wa Simiyu) tuone namna ya kuliweka sawa ili umma uweze kupewa ufafanuzi juu ya mwendelezo wake," aliahidi.

Mkuu wa Wilaya ya Maswa, Aswege Kaminyoge, alikiri kuwa na taarifa za kifo cha kijana huyo. Alisema tayari tayari imeundwa kamati aliyoiita huru kwa ajili ya kuchunguza sababu za kifo cha kijana huyo.

Alisema zipo taarifa za askari polisi kuwa wahusika huku nyingine zikidai aliuawa na wananchi wenye hasira.

Mkuu wa Wilaya alisema kamati hiyo iliyoundwa na serikali haijumuishi askari polisi wala maofisa wa Jeshi la Polisi kwa namna yoyote. Imeanza uchunguzi. Watakaobainika kuwa wahusika wa mauaji hayo watachukuliwa hatua stahiki.

"Tukio hilo lilitokea nikiwa nje kidogo ya wilaya lakini tayari tumefanya hatua za awali na siku ya Ijumaa (jana) ninatarajia kukutana na wananchi wa eneo hilo, lengo likiwa ni kuongea nao na kuwapa pole juu ya msiba huo. Hakuna uvunjifu wa sheria utakaovumiliwa," aliahidi.

Mwandishi alipohoji kama kuna askari polisi waliosimamishwa kazi kupisha uchunguzi huo, Mkuu wa Wilaya huyo alisema hakuna hatua zilizochukuliwa dhidi ya askari yeyote.

Alisema kwa kuwa wote ni watumishi wa umma, ikibainika ni wahusika wa mauaji hao, sheria itachukua mkondo wake.

Eliudi Kabengo ni Mratibu wa Kituo cha Haki za Binadamu wilayani Maswa cha Community Emancipation Organisation (CEO). Amelaani mauaji hayo na wanaendelea kufuatilia kwa karibu hatua zinazochukuliwa.

"Tukibaini ukiukwaji wa haki za binadamu, tutafungua jalada mahakamani na kuweka mawakili wetu kwa ajili ya kusaidia haki inapatikana," alisisitiza Kabengo.

# Fedha za mauzo ya nguruwe zadaiwa chanzo bosi kuuawa

## -Mwili wakutwa katika shimo la choo

**Na Mary Mosha,** ROMBO

MAUZO ya nguruwe ya Sh. 800,000 yametajwa kuchangia kuondoa uhai wa Rogasian Onesfory (60), mkazi wa Kijiji cha Ubetu, Wilaya Rombo mkoani Kilimanjaro.

Hiyo ni baada ya kudaiwa kuuawa kwa kucharangwa mapanga kichwani na mfanyakazi wake wa ndani.

Inadaiwa kuwa mtuhumiwa wa mauaji hayo (jina limehifadhiwa), alipokamilisha dhamira yake, aliutupa mwili wa Rogasian katika shimo la choo nje ya makazi yake.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi Simon Maigwa, alisema jana kuwa mtuhumiwa wa mauaji hayo anasakwa na makachero wao. Alitoroka baada ya kutekeleza mauaji hayo Juni 25 mwaka huu.

"Ni kweli huyu mzee (Rogasian) baada ya kutoka sokoni kuuza nguruwe wake kwa Sh. 800,000, ndipo mfanyakazi wake, akamuua bosi wake na mwili wake wake akautupa katika shimo la choo. Bahati nzuri, tumemfahamu aliyefanya hilo tukio, tutamkamata tu," Kamanda Maigwa alisema.

Kwa mujibu wa Kamanda Maigwa, Jeshi la Polisi lilipokea taarifa za mauaji hayo Juni 27 jioni na saa chache baadaye makachero wake walifika eneo la tukio na kuona eneo kulikofanyika mauaji kumemwagwa maji, huku kukiwa na matone ya damu yaliyofutwafutwa.

"Matone hayo yaliishia chooni na ndipo walipochungulia na kuona kitu kama mguu, waliufuatilia na kisha kuutoa mwili huo. Baada ya kuutoa, ndugu na majirani waliutambua,"alisema Kamanda Maigwa.

Baadhi ya mashuhuda wa tukio hilo, akiwamo Eusebian Tarimo, Walisema kuwa kabla ya kuuawa, alionekana akiwa na nguruwe wake akienda kumuuza mnadani.

"Kama ilivyo kawaida ya huyu mzee, akiwa na fedha si mchoyo, anakaa na wenzake na kupata mbege (pombe) hasa nyakati za jioni.

"Tulijua anazo siku hiyo na baadhi ya wazee walimtafuta bila mafanikio, na hata kujaribu kumpigia simu bila kufanikiwa.

"Kesho yake (siku iliyofuata), baadhi yetu tulikwenda nyumbani kwake kumtafuta kama ulivyo utaratibu wetu, ndipo siku ya pili ikagundulika kwamba aliuawa na mfanyakazi wake. Inauma sana! Tunaviomba vyombo vya dola kuchukua hatua stahiki," alisema Tarimo.

Balozi wa nyumba 10, ambaye pia ni ndugu wa marehemu, Erasmi Onesfory, alimwambia Mwandishi kuwa tangu Juni 25 walijaribu kumtafuta kwa njia ya simu, hakupatikana.

"Baadhi ya ndugu pamoja na majirani walishirikiana kumtafuta bila mafanikio na walipofika nyumbani kwakwe walimkuta mfanyakazi na akawaeleza kuna uwezekano wa mzee huyo amekwenda Dodoma iliko familia yake," alidai.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
01.07.2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Jumatatu tarehe 03-07-2023 kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port** kuelekea Rufiji, gari hizo zina namba za usajili:

**T 624 DFA / T 321 DDH**

**T 167 DFC / T 877 EAU**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:

**Urefu - mita 18.00 Upana - mita 5.00 Kimo - mita 4.60**

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam, Pwani** hadi Rufiji kupitia **Kibiti**, gari zitasafiri muda wa mchana tu (**Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni**)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**


# Wanafunzi UDSM watengeneza gari linalotumia umeme

**Na Joseph Mwendapole**

WANAFUNZI wa Ndaki ya Uhandisi na Teknolojia (CoET) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kwa kushirikiana na wahadhiri wao, wamefanikiwa kutengeneza gari la umeme ambalo halina injini.

Gari hilo limekuwa kivutio katika Maonyesho ya Kimataifa ya Biashara ya 47, maarufu 77, yanayoendelea katika Viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere wilayani, Dar es Salaam.

Akizungumza na wananchi waliotembelea banda la UDSM kushuhudia gari hilo, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Masoko wa chuo hicho, Dk. Dotto Kuhenga, alisema gari hilo limewagharimu Sh. milioni 30.

"Hizo Sh. milioni 30 zinajumuisha gharama za kubuni, ufundi, utaalamu na kila kitu mpaka kukamilika kwake lakini mtu akitaka tumtengenezee kwa sasa, gharama zitashuka na kufikia milioni 10," alisema.

Aliongeza kuwa ingawa katika maonyesho hayo wamepeleka huduma mbalimbali za UDSM, upekee gari la umeme umekuwa kivutio kikubwa na litatumika kubeba viongozi ambao wana shida ya kutembea umbali mrefu kwa miguuu katika maonyesho hayo ya mwaka huu.

"Tumeleta hili gari hapa kuonyesha ubunifu wa vijana wetu wanaosomea uhandisi na teknolojia UDSM na litatumika kutembeza viongozi wenye changamoto ya kutembea kwa miguu katika mabanda mbalimbali.

"Duniani kote magari makubwa huwa hayaruhusiwi kuingia katika viwanja vya maonyesho lakini gari letu ni dogo na ni maalum ambalo linaweza kuwatembeza wageni katika maeneo mengi bila kusababisha usumbufu kwa watu," alisema.

Dk. Kuhenga alisema Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade), walivutiwa na ubunifu huo na kuomba UDSM ipeleka gari hilo katika viwanja hivyo kwa ajili ya kuwatembeza wageni mbalimbali kushuhudia maonyesho hayo kwa urahisi.

"Gari hili liko kwa ajili ya mambo mawili - kuonyesha ubunifu wa wanafunzi wetu wa Ndaki ya Uhandisi na Teknolojia UDSM na kuwatembeza viongozi mashuhuri watakaofika katika viwanja hivi vya Sabasaba," alisema Dk. Kuhenga.

Alibainisha kuwa UDSM iliingia mkataba na Kampuni ya Geita Gold Mine (GGM), ambao walikuwa wakihitaji gari la aina hiyo kwa ajili ya huduma za migodi yao.

Alisema gari hilo linatumia umeme mdogo na kwa raia wa kawaida watakaohitaji gari hilo watatengenezewa kwa Sh. milioni 10.

Alisema gari la kwanza liligharimu Sh. milioni 30 kutokana na maandalizi na michakato mbalimbali ya awali lakini kwa sasa kila watakalotengeneza litagharimu Sh. milioni 10.

"Ni gari rahisi sana kwa mwananchi wa kawaida kwa mfano ukinunua umeme wa Sh. 3,000 unaweza kutembea hadi kilomita zaidi ya 30 na ni ubunifu ambao utasaidia kuachana na matumizi ya mafuta ya petroli," alisema


**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA WA VIFAA CHAKAVU**

i. Wananchi wote mnatangaziwa kwamba Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) utaondosha kwa njia ya mnada wa hadhara mali mbalimbali chakavu zilizokuwa zinatumika kwenye maaeneo ya Utekelezaji wa Mpango.

ii. Mali zitakazouzwa ni vifaa mbalimbali vya ofisi chakavu.

iii. Mnada huo utafanyika katika mikoa mbalimbali kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini:

| Na | Mkoa na Mali zitakazouzwa | Tarehe | Mahali |
|---|---|---|---|
| 1 | Dar es salaam | 8th Julai 2023 | Ofisi za TASAF Tawi la Dar Es Salaam |
| 2 | Mwanza, Dodoma,Iringa Kigoma na Mbeya | 11 Julai 2023 | Ofisi ya Katibu Tawala |
| 3 | Pwani Tanga Manyara Kagera Tabora | 12 Julai 2023 | Ofisi ya Katibu Tawala |
| 4 | Rukwa, Arusha Njombe Mtwara Simiyu Ruvuma | 13 Julai 2023 | Ofisi ya Katibu Tawala |
| 5 | Morogoro Lindi Katavi Shinyanga Geita | 14 Julai 2023 | Ofisi ya Katibu Tawala |
| 6 | Songwe,,Pemba, Killimanjaro, Mara Singida | 18 Julai 2023 | Ofisi ya Katibu Tawala |

**MASHARTI YA MNADA**

i. kifaa kitauzwa kama kilivyo mahali kilipo.
ii. Mnunuzi atalazimika kulipa asilimia mia moja (100%) ya thamani yote na kuondoa kifaa/vifaa atakavyonunua siku ya mnada.
iii. Ruhusa ya kuangalia vifaa itatolewa siku mbili (2) kabla ya terehe ya mnada.
iv. Mnada utaanza saa nne (4:00) Asubuhi katika kila kituo.

Mkurugenzi Mtendaji
Mfuko wa Maendeleo ya Jamii – TASAF
Barabara ya Jakaya Mrisho Kikwete
S.L.P 2719 Dodoma ,Tanzania
simu: 255 026 2963866
Nukushi: 255 026 2963871
Barua pepe: info@tasaf.go.tz
Tofuti: www.tasaf.go.tzg



Kamishna wa Madini, Abdulrahman Mwanga (wa pili kulia), akizungumza na washiriki alipotembelea banda la Geita Gold Mining Ltd kwenye Maonyesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam (DITF), barabara ya Kilwa, mkoani Dar es Salaam, jana. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# Kumekucha miradi mipya mabasi yaendayo haraka

## -Barabara ya Ubungo-Kimara sasa njia nane

**Na Frank Monyo**

SERIKALI imetia saini mikataba minne ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa miundombinu ya mabasi yaendayo haraka (BRT) awamu ya nne kutoka katikati ya mji (Maktaba) hadi Tegeta DAWASA.

Mikataba hiyo pia inajumuisha mradi wa ujenzi wa barabara Mkoa wa Pwani huku ikisisitiza miradi hiyo kujengwa kulingana na thamani ya fedha.

Kati ya mikataba hiyo, umo wa uboreshaji wa miundombinu ya BRT iliyojengwa awamu ya kwanza katika Barabara ya Morogoro ambapo upanuzi utafanyika kutoka Ubungo mpaka Kimara, kipande chenye urefu wa Km tano kwa ajili ya kuongeza njia nane kutoka njia sita za sasa.

Hayo yalibainishwa jana jijini Dar es Salaam na Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Godfrey Kasekenya, wakati wa hafla ya utiaji saini wa mikataba hiyo iliyoshuhudiwa na wawakilishi wa wakuu wa mikoa ya Dar es Salaam na Pwani.

Alisema gharama ya mikataba minne ya BRT ni Sh. bilioni 500.7 huku mkataba wa ujenzi wa barabara mkoani Pwani ukigharimu Sh. bilioni 17.86.

Naibu Waziri alisema awamu hiyo ya nne ni ya ujenzi wa miundombinu ya barabara yenye urefu wa Km 29.13, ikihusisha barabara kutoka katikati ya jiji hadi Tegeta DAWASA na kipande cha kutoka Mwenge hadi Ubungo. Mradi huo unagharimiwa kupitia programu ya Dar es Salaam Urban Transport Project (DUTP).

"Kati ya mikataba ya BRT inayotiwa saini leo (jana), mikataba mitatu inahusu mradi wa ujenzi wa miundombinu awamu ya nne (BRT Phase 4) kutoka Maktaba mpaka Tegeta DAWASA.

"Vilevile, mkataba mmoja unahusu uboreshaji wa miundombinu ya BRT iliyojengwa awamu ya kwanza katika Barabara ya Morogoro ambapo upanuzi utafanyika wa sehemu ya barabara kutoka Ubungo mpaka Kimara yenye urefu wa Km tano kutoka njia sita za sasa kwenda njia nane.

"Kazi nyingine ni kujenga njia za watembea kwa miguu na barabara za pembeni na kuboresha makutano ya barabara kwa kuimarisha barabara za kuwezesha wanaopinda kulia na wanaozunguka kurudi walikotoka (loop roads)," alisema Kasekenya.

Alisema miradi huo pia unahusisha kuweka ngazi kwenye madaraja ya wapita kwa miguu eneo la Kimara na Morocco ili kuweka njia mbadala na kuvutia watumiaji wengi zaidi.

Kasekenya alisema katika mikataba hiyo upo wa ujenzi wa kwa kiwango cha lami barabara ya TAMCO - Vikawe hadi Mapinga; sehemu ya Pangani hadi Mapinga yenye urefu wa Km 13.59 iliyopo mkoani Pwani.

"Barabara hii ina jumla ya Km 22 na inaunganisha barabara kuu mbili za Dar es Salaam hadi Bagamoyo na Dar es Salaam kwenda Morogoro pamoja na mikoa ya magharibi mwa Tanzania na ile ya nyanda za juu kusini," alifafanua.

Alisema ujenzi wa barabara hiyo ni moja ya mikakati ya serikali ya kuharakisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii mkoani Pwani hususani katika Wilaya ya Bagamoyo kwa kuboresha mtandao wa barabara ili kuongeza ufanisi katika sekta ya usafiri na usafirishaji.

Aliongeza kuwa kukamilika kwa barabara hiyo kutachochea ukuaji wa shughuli za kiuchumi kama vile usafirishaji wa mazao ya chakula, mazao ya biashara, mazao ya misitu na shughuli za utalii na za kijamii kwa ujumla.

"Pamoja na manufaa makubwa niliyoyasema, pia inatarajiwa miradi hii itasaidia kutengeneza ajira kwa wananchi wetu wakati wa ujenzi," alisema. Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara (TANROADS), Mohamed Besta, alisema zabuni za ujenzi wa miradi minne ya BRT zilitangazwa kwa uwazi mwezi Septemba mwaka jana (2022) na kufunguliwa mwezi Desemba 2022 na jumla ya zabuni 29 zilipokewa kwa miradi hiyo na kufanyiwa tathmini.

Alimtaja mkandarasi aliyeshinda ni Kampuni ya China Geo - Engineering Corporation kutoka China ambaye atatekeleza ujenzi ujenzi wa miundombinu ya barabara yenye urefu wa Km 13.5 kuanzia Maktaba ya Taifa mpaka Mwenge ikijumuisha kipande cha Barabara ya Sam Nujoma kutoka Mwenge mpaka Ubungo kwa gharama ya Sh. bilioni 174.3.

"Mkataba huu pia unahusisha upanuzi wa Daraja la Selander, ujenzi wa vituo vikuu viwili vya mabasi, vituo vya kawaida vya mabasi 20 na vituo mlisho (Feeder Station) 10. Ujenzi umepangwa kukamilika katika muda wa miezi 18 kuanzia sasa," alisema.

Aliutaja mkataba wa pili kuwa ni ujenzi wa miundombinu ya barabara yenye urefu wa Km 15.63 kuanzia Mwenge mpaka Tegeta, ambapo mkandarasi aliyeshinda zabuni hiyo kuwa ni Kampuni ya Shandong Luqiao Group Co. Ltd kutoka China kwa gharama ya Sh. bilioni 193.8. "Mkataba huu pia unahusisha upanuzi wa madaraja matatu (Mlalakuwa, Kawe na Tegeta), ujenzi wa vituo vikuu vya mabasi, vituo vya kawaida vya mabasi 19 na vituo mlisho vitano. ujenzi umepangwa kukamilika katika muda wa miezi 18," alisema.

Aliongeza: "Mkataba wa tatu ni ujenzi wa Karakana mbili na kituo kikuu cha mabasi kimoja. Mkandarasi aliyeshinda ni Kampuni ya China Communications Construction Company Ltd kutoka China kwa gharama ya Sh. bilioni 60.9. Ujenzi umepangwa kukamilika katika muda wa miezi 18," alisema.

Aliutaja mkataba wa nne ni wa uboreshaji wa miundombinu ya barabara na upanuzi wa sehemu ya barabara ya Ubungo hadi Kimara Km tano kutoka njia sita hadi njia nane kwa lengo la kuongeza usalama wa watumiaji wa barabara.

"Mkandarasi aliyeshinda ni Kampuni ya Sichuan Road & Bridge (Group) Corporation Ltd kutoka China kwa gharama ya Sh. bilioni 71.4. Ujenzi umepangwa kukamilika katika muda wa miezi 18," alisema.

Besta alimtaja mkandarasi aliyeshinda tuzo ya ujenzi wa barabara kiwango cha lami mkoani Pwani kutoka TAMCO - Vikawe hadi Mapinga kwa kiwango cha lami; sehemu ya Pangani hadi Mapinga (Km 13.59) kuwa ni Kampuni ya Kings Builders Ltd ya Tanzania.

"Mradi huu utajengwa kwa gharama ya Sh. bilioni 17.8 bila kujumuisha Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ya Sh. bilioni tatu. Muda wa utekelezaji wa mradi ni miezi 12," alisema.

## Operesheni yanasa 23 tuhuma uvuvi haramu

**Na Romana Mallya**

KITENGO cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU) kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Kikosi cha Wanamaji, wameendesha operesheni maalum ya kukabiliana na uvuvi haramu maeneo tengefu na kukamata mitumbwi ya wavuvi na watuhumiwa 23.

Meneja wa MPRU, Dk. Immaculate Semesi, akizungumzia operesheni hiyo iliyoendeshwa katika maeneo tengefu kwa kuhusisha visiwa mbalimbali, alisema lengo lake ni kutokomeza uvuvi haramu unaotumia vilipuzi.

"Kwanini tunasisitiza huu ni uvuvi haramu na uharibifu mkubwa? Uvuvi huu wa kutumia vilipuzi hufanywa katika maeneo mahususi kwa ajili ya kuzalisha rasilimali za mazao ya uvuvi," alisema.

Meneja huyo alisema uharibifu namba moja unaofanywa kwa kutumia vilipuzi husababisha kuhatarisha maisha ya wanaotumia vilipuzi hivyo na jamii husika, kwa kuwa huharibu mazao hayo ya chakula na ya biashara.

Pia huhatarisha utalii pamoja na pwani, husababisha uharibifu wa mazingira na kusababisha kuchukua muda mrefu kurudi katika hali ya kawaida au visirejee kabisa.

"Ni kama unatengeneza jangwa ndani ya maji. Kazi yetu namba moja ni kuelimisha jamii juu ya uhifadhi na umuhimu wa rasilimali bahari na kuchukua juhudi mbalimbali za kudhibiti uhalifu wa aina yoyote baharini. Sisi kama chombo cha serikali tumeshirikisha wenzetu wa ulinzi na usalama kusaidia zoezi hili," alisema.

Kamanda wa Polisi wa Kikosi cha Wanamaji, Kamishna Msaizidi Moshi Sokoto, alisema operesheni hiyo ambayo ni endelevu ilianza Juni 17 mwaka huu na kukamata mitumbwi minne ya wavuvi na watuhumiwa 23 ambao utaratibu wa kuwafikisha mahakamani unaendelea. "Wavuvi saba ni wavuvi haramu kwa kutumia baruti, hawa walifanikiwa kukimbia kuelekea pwani. Kwa sababu yalikuwa ni mazingira ya jioni, tunaendelea kufuatilia nyendo zao, vyombo vyao tumevikamata. Nyavu na vielelezo vingine tumevikamata," alisema.

Aliongeza kuwa watuhumiwa wengine walikamatwa wakiwa na makokoro yanayovua maeneo tengefu ambayo ni sehemu ya mazalia ya samaki.

Kamanda huyo alitoa rai kwa wavuvi wafahamu vitendo wanavyovifanya ni kosa kisheria kwa kuwa wanadidimiza uchumi wa nchi kwa kuua viumbe wachanga na mazalia yake. "Tumemsikia Rais Samia Suluhu Hassan, amesema nchi inakwenda kwenye uchumi wa buluu. Tutaendaje huku tunafanya uvuvi haramu? Lazima tuache. Tunatoa elimu kwao na kama ikishindikana kuacha kwa hiari, tutawakamata kama hivi," alionya.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tusilipuuzie soka la vijana

**MARA** baada ya msimu wa ligi kuu wa 2022/2023 kumalizika mwezi uliopita, ilianza michuano ya vijana wenye umri wa chini ya miaka 20 wa vilabu vya ligi kuu.

Jana tulishuhudia michezo ya nusu fainali ya ligi hiyo ambayo inaenda ukingoni kwa sasa.

Kwanza tuwapongeze Shirikisho la soka Tanzania (TFF) kwa angalau kuja na mashindano haya muhimu kwa mustakabali wa mafanikio ya mchezo huu kwa nchi yetu.

Tunafahamu TFF ina maono mazuri juu ya kuwepo kwa ligi nzuri na yenye ushindani kwa vijana, inawezekana wanakwamishwa na hali ya uchumi.

Kuendesha ligi yoyote iwe ya vijana, watoto au ligi ya wanawake inahitaji kuwepo kwa pesa za uendeshaji ambazo zitazisaidia klabu kushiriki kikamilifu michuano hiyo.

Ni kweli TFF peke yake kama taasisi ya kusimamia mpira hapa nchini haiwezi kufanya mambo yote haya peke yake bila kupata uwezeshwaji sehemu.

Ni wito kwa wadau wote wa soka kuanzia makampuni, mashirika na hata taasisi za Serikali kugeukia soka la vijana kwa kuwasaidia TFF kuendesha ligi iliyokamilika ya vijana.

Soka la vijana ndio msingi wa maendeleo ya soka, ndio msingi wa timu yetu ya Taifa ya baadae, kama kweli tunataka kufanya vizuri kwenye soka ni lazima kuweka misingi imara kwenye soka la vijana.

Ligi inayoendeshwa sasa haitoshi kwa sababu ni ligi inayofanyika mara baada ya ligi kuu kumalizika, tunapaswa kuwa na ligi yetu iliyokamilika ya vijana ambayo watashiriki kwa msimu mzima.

Lakini ili jambo hili lifanyike na kufanikiwa ni lazima wadau kuungana na TFF kusaidia kudhamini ili iendeshwe kama ligi iliyokamilika na sio kama sasa hivi inafanyika kwa wiki chache tu.

Faida ya ligi rasmi ya vijana sio tu kwa timu yetu ya Taifa, bali pia kwa vilabu vyetu ambavyo sasa vitakuwa na 'shamba' la kuvuna wachezaji watakaowatumia kwenye ligi kuu.

Hii itawapunguzia pia gharama ya kusajili wachezaji wakubwa kutoka kwenye vilabu vingine au nje ya nchi, watakuwa wakiwapandisha wachezaji wao vijana.

Duniani kote soka la vijana ndio msingi wa kuwa na klabu bora na imara yenye mfumo wake maalum, tunayashuhudia haya kwenye klabu za Ulaya.

Kuanzia Manchester United pale England, Barcelona kule Hispania au Bayern Munich kule Ujerumani, wote wamewekeza kwenye soka la vijana ambalo baadae baada ya kukomaa wanawapandisha kwenye timu kubwa au kuwauza kwenye timu nyingine na kujiingizia pesa.

Hii inawezekana kwa vilabu vyetu vya hapa, Simba na Yanga, angalau Azam tayari wameanza kuonyesha muelekeo huo lakini sasa inatakiwa kuwepo kwa ligi ya vijana iliyokamilika.

Taasisi, Makampuni na Mashirikia haya yanayodhamini Ligi kuu au vilabu vya ligi kuu, wanaweza wakageukia soka la vijana na kuamua kudhamini ili kuwa na Ligi bora ya vijana ya msimu mzima.

Tuwekeze kwenye soka la vijana, mitaani kuna wachezaji wengi vijana lakini hawana sehemu ya kuonyesha vipaji vyao, kuwepo kwa ligi imara ya vijana itaibua wachezaji wengi sana ambao baadae wanaweza wakaja kuwa wachezaji muhimu kwa taifa letu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Tuzalishe kwanza wachezaji waliokamilika ndipo tupunguze idadi ya wageni Ligi kuu

Na Adam Fungamwango

**ULE** mjadala ambao wa mara kwa mara wa kupunguza wachezaji wa kigeni kwenye Ligi ya Tanzania umeonekana kujirudia tena.

Sitaki kwenda mbali sana, lakini mashabiki wengi wa Tanzania wanajua kama si wachezaji wa kigeni, klabu ya Simba isingeweza kufika hatua ya robo fainali kimataifa, mara tata Ligi ya Mabingwa na mara moja Kombe la Shirikisho.

Wachezaji kama Meddie Kagere, Emmanuel Okwi, Haruna Niyonzima, James Kotei, Sadio Kanoute, Thadeo Lwanga, Zana Coulibaly, Chriss Mugalu, Jean Baleke, Saido Ntibazonkiza, na wengineo, wamekuwa mbele ya mafanikio haya, wakichagizwa na Wabongo wachache tu kina Jonas Mkude, Aishi Manula, Shomari Kapombe, John Bocco na Mohamed Hussein 'Tshabalala.'

Yanga isingeweza kufika fainali za Kombe la Shirikisho kama si kina Fiston Mayele, Kennedy Musonda, Djuma Shaaban, Joyce Lomalisa, Yannick Bangala, Jesus Moloko, Tuisila Kisinda, Stephane Aziz Ki, Khalid Aucho na wengineo.Watanzania wachache waliopo kwenye mafanikio hayo ya Yanga ni Bakari Mwamnyeto, Kibwana Shomari, Mudathir Yahaya na Dickson Job kwa uchache.

Wabongo tukubali tusikubali kama isingekuwa wachezaji hawa wa kigeni, klabu zetu zingekuwa zinatolewa kwenye hatua za awali au raundi ya kwanza kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa au Kombe la Shirikisho kama ilivyokuwa miaka kadhaa iliyopita.

Hata huko nyuma ni miaka michache michache tu, tena baada ya kupita miaka mingi ndiyo klabu zetu zinafanya vyema michuano ya kimataifa, halafu inaweza kupita hata miaka 10 na zaidi ndiyo ijirudie.

Leo hii imefika wakati mashabiki wanaona Simba kufika robo fainali mara nne mfululizo ni kama wamefeli hivi, wakati haijawahi kutokea tangu historia ya klabu hiyo kutinga hatua hiyo mfululizo. Ni kwa sababu ya wachezaji wa kigeni inaowasajili.

Kuwapunguza ni kujipiga risasi mguuni, kwani tunaweza kujidanganya tu hapa kwenye ligi kwamba wachezaji wa Kitanzania wanacheza vizuri, lakini matokeo yanaonekana kwenye michuano ya kimataifa.

Mimi nadhani kuwapunguza wachezaji wa kigeni ni kutaka kulirudisha nyuma soka la Tanzania. Tunawapunguzaje wachezaji wa kigeni, mbona hata ukihesabu idadi ya Wabongo ni wengi zaidi kwenye Ligi Kuu kuliko wageni?

Tunaona ni wengi kwa sababu wao ndiyo wanawika kwa kujituma zaidi kwa sababu wamekuja kutafuta na wanajitambua huku wakiwa na mwendelezo mzuri.

Mchezaji wa Kitanzania akianza kuwa staa, anaanza maringo na kupunguza kujituma kwenye mazoezi, lakini Mayele kila siku anafunga na anazidi kuwa 'mtamu' kama mcharo kwa sababu habweteki, anazidi kujituma zaidi.

Kina Ntibazonkiza, pamoja na kwamba umri umekwenda lakini ana namba nyingi nzuri za pasi za mabao pamoja na kufunga tofauti na viungo vijana wa Tanzania.

Tutake tusitake wachezaji wengi wa Kitanzania hawajakamilika kiushindani, na kama kweli wangekuwa wamekamilika wala tusingekuwa tunalialia kuwatafutia au kuwatengenezea kanuni za kuwalinda, wasingehitaji kanuni.

Tungewaona wetu wametoka nchini kwenda kucheza soka la kulipwa nje ya nchi lakini tangu atoke Mbwana Samatta na Simon Msuva ni wachache sana waliofuatia.

Waliobaki wanasubiri huruma ya kanuni, kama klabu ina wachezaji 30, halafu 12 wanakuwa wa kigeni, kwa nini 18 wa Kibongo wasitawale? na hata wao 12 wanaoweza kumudu kusajili wote hazizidi timu nne.




Mkurugenzi na Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Chakula Duniani (WFP), Sarah Gordon-Gibson (kulia) akikabidhi mashine ya kutolea nakala kwa Mkurugenzi wa Huduma za Wakimbizi wa Wizara ya Mambo ya Ndani, Sudi Mwakibasi jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: FAUSTINE FELICIANE**

## KESI MAGUNIA MKAA

# 'Viatu chakavu vilitumika katika kuchoma mwili mke aliyeuawa'

**Na Grace Gurisha**

MSHITAKIWA Khamis Luwonga (38), anayetuhumiwa kumuua mke wake, Naomi Marijani na kumchoma moto kwa kutumia magunia mawili ya mkaa, anadaiwa kutumia viatu chakavu kuuchoma moto mwili wa mkewe, ikiwa ni mbinu ya kupoteza harufu ya binadamu.

Imedaiwa mahakamani kuwa baada ya kumpiga mke wake na ubapa wa mkono mithili ya kareti na kudondoka chini, Naomi alimwomba mume wake amsamehe na Mungu pia amsamehe, maneno ambayo yalimchanganya mshitakiwa ndipo alipoamua kumchoma moto.

Mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Ramadhani Rugemarila wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam jana, Wakili wa Serikali, Mosie Kaima, alidai hayo aliposoma maelezo ya mashahidi na vielelezo katika kesi hiyo kabla jalada halijapelekwa Mahakama Kuu.

Akiendelea kusoma maelezo hayo ya mashahidi 28, Kaima alidai mshitakiwa amekiri kumuua mke wake na kuuchoma moto mwili wake na kisha kufukia majivu yake shambani kwake Mkuranga mkoani Pwani.

Alidai kuwa baada ya kupata wazo hilo, aliamua kuhamisha kuku kutoka katika banda na kuwaweka sehemu nyingine ambako pembeni ya banda hilo kulikuwa na shimo.

"Alimtafuta kijana wake ambaye alikuwa anamtuma kazi, alimwelekeza aende kwa wakala amtumie namba ili atoe fedha.

Alitoa Sh. 100,000 akamwambia aende akanunue gunia moja la mkaa, akiwa njiani alikutana na mtu anauza mkaa akiwa ameubeba kwenye baiskeli.

"Alinunua gunia moja Sh. 45,000 na kisha akasaidiana na muuzaji huyo na kuliingiza ndani ambapo mshitakiwa aliwataka waliache njiani wasilipeleke jikoni, walikuta gunia lingine la mkaa lipo," alidai Kaima.

Kaima alidai kuwa mshitakiwa alimpigia simu dereva bodaboda na kumweleza kuwa, amletee mafuta ya taa lita tano, akishayafikisha ndipo atakapomlipa. Alimlipa Sh. 12,000 akaondoka.

Alidai kuwa, shahidi mwingine, aliagizwa gunia la pili, alikwenda kulinunua Sh. 46,000 siyo mbali na eneo analoishi mshitakiwa, ambapo mshitakiwa alimweleza kwamba, gunia hilo waliache nje wasiliingize ndani.

Aliendelea kudai kuwa mshitakiwa alitanguliza mkaa kwenye shimo ambalo lilichimbwa na wajomba zake. Lilikuwa karibu na banda la kuku na kisha kuutumbukiza mwili wa marehemu Naomi na kuweka mkaa mwingine juu yake na kisha kuwasha moto huku akichochea kwa viatu.

"Alikuwa akichochea moto kwa viatu kwa lengo la kupoteza harufu ya mwili wa binadamu na pia wakati mkaa huo ukipungua, mshitakiwa alikuwa akiongeza mwingine huku akiuchochea," alidai Kaima.

Aliendelea kudai kuwa mshitakiwa Luwonga baada ya kumaliza tukio hilo, alikusanya majivu katika viroba viwili na kuviweka kwenye gari lake na kisha kuvipeleka shambani kwake Mkuranga na kuvifukia chini huku juu alipanda mgomba.

"Kabla ya kufika huko, mshitakiwa alimwagiza kijana ambaye anamsafishie shamba lake hilo, kwamba achimbe mashimo matatu ambapo anataka kupanda minazi. Alifanya hivyo na alilipwa Sh. 30,000.

"Wakati uchunguzi ukiendelea, mshitakiwa alikamatwa na kueleza kwamba, yeye ndiye alimuua mke wake kwa bahati mbaya na kisha kuuchoma mwili wake moto na kufukia majivu yake.

"Kutokana na msukumo wa Roho Mtakatifu aliyemshukia mshitakiwa, aliamua kusema ukweli kwamba, yeye ndiye kamuua Naomi na taarifa aliyoitoa kuwa mke wake katoweka nyumbani siyo ya kweli,"

"Mshitakiwa alikuwa mwazi sana na alitoa ushirikiano kwa kuonyesha shimo alipomchomea mke wake na alipokwenda kuyafukia shambani kwake Mkuranga," alidai.

Mshitakiwa aliwapeleka polisi eneo alipomchomea mke wake na kuwaeleza kuwa baada ya kumsukuma ukutani akadondoka chini alipasuka kichwani na damu nyingi zilitoka, ambapo alianza kufuta damu hizo kwa kupoteza ushahidi.

Walipofika shambani kwake Mkuranga, mshitakiwa aliwaonesha alipofukia majivu ya mke wake, ambapo mgomba uling'olewa na yalikutwa majivu viroba viwili yalipochambuliwa kulikutwa na mifupa midogo iliyoungua kwa kiwango kikubwa. Pia waliona meno.

Katika kesi hiyo ya muuaji Na. 4 ya mwaka 2019, mshitakiwa Luwonga ambaye ni Mkazi wa Kigamboni, Dar es Salaam, anadaiwa kuwa Mei 15, mwaka 2019, akiwa Gezaulole, Kigamboni, alimuua Naomi Marijani.

# PSSSF yavipa vifaa tiba vituo vya afya

**Na Mwandishi Wetu,** BUTIAMA

MFUKO wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) umetoa msaada wa vifaa tiba kwa vituo sita vya afya ili kuwaunga mkono watumishi wa umma katika kutoa huduma za afya kwa wananchi.

Vituo vilivyonufaika na msaada huo ni pamoja na Kituo cha Afya Kirumi kilichoko Wilaya ya Buatiama mkoani Mara ambacho kilikabidhiwa vifaa jana na Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF, Hosea Kashimba.

Katika hafla fupi ya kukabidhi vifaa hivyo, Kashimba alivitaja vituo vingine vitano vya Mkunguni na Dimbani vilivyoko Kizimkazi (Zanzibar), Ikombe, Mtwara, Mji vya mkoani Lindi na Ilembo cha mkoani Katavi, vimenufaika na msaada huo. Ni vifaa vilivyotolewa wakati wa kilele cha maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma mwaka huu.

"Hapa tuko mahala pake, nyote ni watumishi wa umma, mko hapa kuihudumia jamii ya Kirumi, tunaamini vifaa hivi tulivyokabidhi vitasaidia kuimarisha utoaji wa huduma bora kwa wagonjwa wetu," alisema Kashimba, ambaye alifuatana na Meneja wa Kanda ya Ziwa, Rajab Kinande, Meneja Uhusiano na Elimu kwa Wanachama, James Mlwoe na Meneja wa Mkoa wa Mara, Nyaswi.

Kashimba aliipongeza serikali chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kufanya mapinduzi makubwa katika sekta ya afya nchini.

"Tunashuhudia maendeleo makubwa ya ujenzi wa miundombinu ya afya kila pembe nchini, ni wajibu wetu kama taasisi ya umma kuunga mkono mafanikio haya makubwa ya serikali," alisema mkurugenzi huyo.

Akifafanua zaidi, alisema Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) ilitoa maelekezo kwa taasisi za umma kuangalia namna bora ya kuadhimisha Wiki ya Utumishi wa Umma kwa kuwatemebea watumishi wa umma walio pembezoni mwa nchi ili kujua changamoto wanazokabiliana nazo katika kutoa huduma kwa wananchi.

"Kubwa ni kuwasisitizia watumishi kuhusu uwajibikaji mahali pa kazi na eneo ambalo tulilichagua ni eneo la afya na hii ni kwa kutambua huduma za afya ni moja ya mahitaji muhimu ya kila binadamu.

"Kuimarisha utoaji huduma za afya ni kujenga jamii iliyo na afya bora na hivyo kupelekea kulinda nguvu kazi na hatimaye kuchangia uzalishaji na kuleta maendleo ya Taifa," alisema.

Katibu Tawala Mkoa wa Mara, Msalika Makungu, aliishukuru PSSSF kwa kuwaunga mkono kwa kutoa vifaa tiba.

"Tunaamini kwa msaada wenu kuwaunga mkono, mnawatia nguvu si watumishi tu bali pia wananchi ambao kwa nguvu zao ndio waliojenga kituo hiki cha afya," alifafanua Msalika.

Alitoa wito kwa viongozi na wananchi kuvitunza na kuwa walinzi wa vifaa tiba walivyopokea.

"Hivi karibuni katika baadhi ya maeneo hapa nchini kumetokea wizi wa vifaa tiba katika vituo vyetu vya kutolea huduma za afya, na vifaa hivyo vinapoibiwa na watu wasio waaminifu, wasiojali matokeo ya vitendo vyao, kunakuwa na changamoto kubwa ya utoaji wa huduma.

"Tuhakikishe yaliyotokea kwingine yasitokee hapa Kirumi na kwa kufanya hivyo tunawapa nguvu na moyo hawa wanaotusaidia kwa sababu wangependa kuona wananchi wanafaidika katika utoaji wa huduma," aliagiza. Msalika pia aliwaomba wananchi kuwa walinzi wakuu kwa kuwa wahalifu hawawezi kufika kijijini bila kuwa na wenyeji.



Mwenyekiti wa Baraza la Usimamizi wa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, Dk. Naomi Katunzi (kulia), akiwatunuku wahitimu vyeti vya kuhitimu elimu ya watu wazima katika mahafali ya 60 yaliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Serikali kuwakabidhi nyumba walionunua Morocco Square

**Na Romana Mallya**

SHIRIKA la Nyumba la Taifa (NHC) limesema leo linatarajia kuwakabidhi wananchi nyumba zao walizonunua katika mradi mkubwa wa Morocco Square uliopo Wilaya ya Kinondoni, Dar es Salaam baada ya kukamilika.

Mkuu wa Kitengo cha Habari na Uhusiano wa NHC, Muungano Saguya, alimwambia mwandishi jana kwamba Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula, anatarajiwa kuwakabidhi wananchi nyumba zao walizonunua katika mradi huo.

Morocco Square ni miongoni mwa miradi mikubwa ya NHC. Una ukubwa wa mita za mraba 110,000.

Mwezi Juni mwaka 2021, Nipashe iliripoti kuhusu kusimama kwa mradi huo kwa miaka minne. Ulianza kutekelezwa Juni 2014 na ulitarajiwa kukamilika mwanzoni mwa mwaka 2017.

Mradi huo ulisimama mwaka 2017 baada ya ujenzi wake kusuasua kuanzia mwaka 2015 kutokana na wanunuzi wa mauzo ya kabla ya jengo kupungua.

Mradi huo ambao unatajwa kuwa mkubwa zaidi wa nyumba Afrika Mashariki na Kati, ujenzi wake unatarajiwa kugharimu Sh. bilioni 137.5.

Miradi mingine ambayo wakati huo ilikuwa imesimama ni pamoja na wa Kawe unaoitwa Seven Eleven (711) wenye thamani ya Sh. bilioni 105.

Shirika hilo pia lina mradi wa Golden Premier Residence (GPR) ulioko Barabara ya Mwai Kibaki wenye thamani ya Sh. bilioni 71.

Kijiografia, mradi huo uko mbele ya ule wa Kawe 711 na mradi wa nne ni ulioko katika Kiwanja Na. 300 (Ada Estate) wenye thamani ya Sh. bilioni 24.2.

# Kampuni yatoa msaada kwa wanafunzi wa kike

**Na Lulu Mussa,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, amepokea maboksi 84 ya taulo za kike kutoka kwa kampuni ya DoweiCare ambao ni watengenezaji na wasambazaji wa taulo hizo kwa ajili ya kuratibu ugawaji kwa wanafunzi wa shule mbalimbali katika Mkoa wa Dodoma.

Akipokea taulo hizo jana, Senyamule aliishukuru kampuni hiyo kwa msaada wa taulo hizo. Zitasaidia watoto wa kike kuwasitiri na kuwezesha kuhudhuria masomo bila kikwazo chochote.

"Ninawashukuru sana kwa kujali makundi yenye uhitaji, ni mchango mkubwa kwa Mkoa wa Dodoma hususan kwa wazazi ambao hawana uwezo wa kuwezesha ununuzi wa taulo za kike.

"Tutahakikisha tunawapa walengwa ambao ndio wahitaji hasa wenye mazingira magumu." Senyamule alisisitiza.

Alisema atawasisitiza wanafunzi wanufaika wa taulo hizo kusoma kwa bidii ili kazi inayofanywa na kampuni ya kusambaza taulo hizo iwe na manufaa na kuonyesha kuwa msingi mkubwa ni wao kupata elimu.

Ofisa Taaluma Mkoa wa Dodoma, Jane Mangowi, alisema taulo hizo pia zitasaidia wanafunzi wenye uhitaji kufikia malengo tarajiwa huku akitoa rai kwa wadau wengine kujitokeza zaidi kusaidia kwa kuwa mahitaji bado ni mengi.

Ofisa Masoko wa Kampuni ya Doweicare, Geoffrey Duma, alisema wako tayari kuendea kushirikiana na Ofisi ya Mkuu Mkuu wa Mkoa wa Dodoma kuchangia taulo zaidi.

Kampuni ya DoweiCare Technology Limited imetoa taulo za kike zenye thamani ya Sh. milioni 2.6.

# Waziri aagiza mgodi wa almasi uanze uzalishaji

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MGODI wa almasi (Wiliamson Diamond) uliopo Mwadui wilayani Kishapu mkoani Shinyanga uliosimama kwa takriban miezi minane baada ya bwawa la kuhifadhia tope kupasuka, unatarajiwa kuendelea na shughuli zake mwezi huu.

Novemba 7 mwaka jana, kingo za bwawa la kuhifadhi maji tope zilipasuka na kuyatiririsha kwenye makazi ya watu, hivyo kusimamisha shughuli za uzalishaji madini.

Akiwa ziarani mkoani hapa jana, Waziri wa Madini, Dotto Biteko, alisema kwa maelezo ambayo amepewa kuhusu ujenzi wa bwawa hilo, asilimia kubwa limeshakamilika na lipo tayari kutumika.

Waziri huyo aliagiza hadi kufikia Julai 15 mwaka huu, uzalishaji wa almasi uanze mara moja.

"Kusimama kwa mgodi huu mara baada ya kupasuka kwa bwawa la kuhifadhia maji tope kumesababisha serikali kukosa mapato mengi sana, na sekta ya madini hapa ndiyo inayoongoza kwa kuingiza fedha za kigeni, tunataka hadi Julai 15 shughuli za uzalishaji zianze," aliagiza.

Waziri Biteko pia aliagiza mgodi huo ukamilishe ulipaji fidia kwa wananchi watano waliosalia ili kusiwapo na malalamiko ya aina yoyote bali kila mtu aridhike na fidia ambayo amepewa.

Mbunge wa Kishapu, Boniphace Butondo, aliipongeza serikali na mgodi huo kwa hatua ambazo inaendelea kuzichukua tangu kupasuka kwa bwawa hilo, kwa kulipa fidia na kuwatimizia wananchi mahitaji yao yote tangu walipopatwa na maafa hayo.

Alisema kuanza kwa shughuli za uzalishaji ni faraja kubwa kwa wananchi wa Kishapu pamoja na halmashauri kupata mapato kupitia ushuru wa huduma, fedha ambazo zitatekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Meneja Mkuu wa Mgodi wa Almasi Mwadui, Ayoub Mwenda, alisema ujenzi wa bwawa jipya mgodini hapo umekamilika kwa asilimia 97 na lipo tayari kwa matumizi. Kinachokuwa kinasubiriwa ni kibali ili wawashe mitambo.

Kuhusu fidia, alisema wameshalipa kwa asilimia 96 na wameshashughulikia pia malalamiko ya wananchi 61 ambao walikuwa hawajaridhika na fidia na sasa kumesalia watu watano.

Alisema wanatarajia mwezi huu kujenga nyumba 47 za wananchi ambao walipoteza makazi yao na fidia zingine za mashamba na upotevu wa vitu mbalimbali vya ndani tayari wameshawalipa.



## HABARI DODOMA

# TIA yaonyesha dawa ya mmomonyoko wa maadili

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKURUGENZI wa Taasisi ya Uhasibu on Tanzania (TIA) Kampasi ya Singida, Dk. James Mrema, amewataka washauri wa wanafunzi kutoka vyuo vya elimu ya juu, vya kati, vya ufundi na viongozi wa serikali za wanafunzi wametakiwa kupanga mbinu za kuwalinda vijana ili kukabiliana na tatizo la mmomonyoko wa maadili nchini.

Dk Mrema alitoa kauli jana mjini hapa alipomwakilisha Ofisa Mtendaji Mkuu wa TIA katika mafunzo kwa washauri hao yaliyoandaliwa na Chama cha Ushauri na Uelekezi kwa Washauri wa Wanafunzi Vyuo vya Elimu ya Juu Tanzania (TACOGA 1984).

Alisema mmomonyoko wa maadili kwa vijana umekuwa tatizo kubwa katika jamii ya watanzania na inarudisha nyuma maendeleo ya taifa, hivyo ni muhimu mafunzo hayo yalenge kupanga mbinu za kuwalinda vijana.

Mwenyekiti wa TACOGA1984, Sophia Nchimbi, alisema kazi kubwa wanayoifanya ni kutoa ushauri nasaha kwa wanafunzi na kwa wafanyakazi, kutoa mafunzo kwa serikali za wanafunzi na kwa sekondari kuhusu mambo mbalimbali.

Alisema chama hicho kilianzishwa rasmi mwaka 1984. Vyuo vilivyoshiriki mafunzo hayo ni 39 kutoka Tanzania Bara na Zanzibar.

Alisema kati ya kazi ambazo wanazifanya ni kutoa ushauri na unasihi katika ofisi zao na nje wadau wao wakubwa wakiwa ni wanafunzi, wafanyakazi na wengine kutoka nje ya ofisi zao na pia wanatoa mafunzo ya namna hiyo kwa serikali za wanafunzi wa vyuo binafsi na shule za sekondari na kuwafundisha shughuli za mapambano ya kutokomeza ukatili.

Alitaja kazi nyingine wanazozifanya ni utafiti na pindi wanapokutana katika mikutano yao ya kila mwaka huwa wanabadilishana uzoefu kwa kuwa mara nyingi wanapoifanya peke yao inakuwa ngumu.

Alisema mafunzo yaliyotolewa ni kudhibiti migogoro ya wanafunzi katika vyuo, uongozi wa wanafunzi na usimamizi wa mabadiliko, ukatili wa kijinsia, kupunguza ukeketaji wa kijinsia vyuoni na kwa wanafunzi kwa ujumla na matatizo ya afya ya akili.

Mengine ni ustawi miongoni mwa wanafunzi, Virusi vya Ukimwi (VVU) na Ukimwi na masuala mtambuka, usimamizi wa fedha za wanafunzi, bajeti, utunzaji wa fedha na ukaguzi, huduma kwa wateja, kusimamia na kuboresha miongozo ya ushauri nasaha.

Alisema pamoja na kazi hizo nzuri wanazozifanya, kuna changamoto kadhaa zikiwamo za ushiriki mdogo wa wadau wao na vyuo kutoka Wizara ya Elimu, vyuo vya kati na vyuo vya VETA ambapo wakizungumza nao moja kwa moja wanataka kwanza wazungumze na wizara husika kwa ajili ya kupata kibali.

## SERA, MITAALA MIPYA ELIMU

# JK ataka ubora wahitimu umulikwe

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS mstaafu Jakaya Kikwete, maarufu JK, ameshauri katika mabadiliko ya Sera ya Elimu na mitaala, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia itilie mkazo suala la ubora ili kukidhi mahitaji ya soko kitaifa na kimataifa.

Kikwete ambaye ni Mwenyekiti wa Mfuko wa Ushirika wa Wafadhili wa Elimu Duniani (GPE), alitoa ushauri huo hivi karibuni katika kikao na wizara hiyo cha kumpitisha kwenye Rasimu ya Sera ya Elimu na Mafunzo Mwaka 2014 toleo la 2023 na mabadiliko ya mitaala.

Alisisitiza mabadiliko hayo yaakisi Malengo Endelevu ya Maendeleo ya Dunia kwa kutoa elimu bora kwa wote na kuhakikisha ubora wa wahitimu katika ngazi zote.

"Mageuzi haya ni ya msingi. Ninaomba tuzingatie sana suala la ubora. Na katika utekelezaji hakikisheni umma wa watanzania unaelimishwa, mweleze kuhusu manufaa yake sasa na hata baadaye," alisema.

Aliahidi kuendelea kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia katika kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali za kutekeleza mageuzi hayo kwa kushirikisha wadau mbalimbali.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alimshukuru Kikwete kwa kutoa maoni kuhusu mwelekeo huo mpya wa sera ya elimu na mitaala.

"Tunapoanza utekelezaji hasa upande wa amali, tunaanza kwa ubora wa hali ya juu, ndio maana tunahitaji sana ushiriki wa wadau," alisema.

Prof. Mkenda alimhakikishia kiongozi huyo kuwa wizara imejipanga kikamilifu katika kutekeleza kwa awamu malengo yote ya sera baada ya kupitishwa rasimu hiyo kulingana na



Waziri wa Maji, Jumaa Aweso (kushoto), akizungumza na Mbunge wa Jimbo la Ulanga, Salim Hasham aliyemtembelea ofisini kwake, jijini Dodoma jana ambapo walizungumza maendeleo ya sekta ya maji. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Asilimia 66 watoto Jangwa la Sahara si watimilifu kiakili

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

IMEELEZWA kuwa asilimia 66 ya watoto kuanzia umri wa siku 0 hadi miaka minane katika jangwa la Sahara si watimilivu wa akili katika uzalishaji utakaochochea uchumi wa nchi.

Mratibu wa Mradi wa Watoto Wetu Mkoa wa Dodoma, Frank Samso, alibainisha hilo alipomwakilishi Mkurugenzi wa Children in Cross Fire, katika mafunzo ya Kitaifa ya Sayansi ya Malezi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto yanayofanyika jijini Dodoma chini ya mradi wa Mtoto Kwanza kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia ,Wanawake na Makundi Maalum.

Alisema asilimia 47 ya watoto wenye umri huo ndio wenye utimilifu wa akili na kushauri ili kuwa na Taifa bora lazima kuwekeza katika akili ya mtoto akiwa na umri huo.

"Ukimwandaa mtoto kiakili kwa kuanzia umri wa siku 0 hadi miaka minane, utakuwa umewekeza kwa mtoto kwa asilimia 96, jambo ambalo litawezesha taifa kuwa na watoto wenye akili na wenye uwezo mkubwa wa uzalishaji kutokana na kuwa na utimilifu wa akili bora kulinganisha na watoto ambao watakuwa hawajaandaliwa vyema katika utimilifu wa akili," alisema.

Mkurugenzi wa Mtandao wa Makuzi ya Mtoto Tanzania (TECDEN), Mwajuma Rwebangila, alisema wamedhamiria kuwezesha maboresho ya malezi ya mtoto na kuongeza utaalamu kwa wataalamu kitaifa kwa kufanya mafunzo kikamilifu kutoka kwa watoto asilimia 26 hadi kufikia asilimia 53 kwa utimilifu wa akili. Alieleza kuwa mtandao huo umekuwa ukihamasisha zaidi jamii kujua umuhimu wa kuwapo kwa uboreshaji wa malezi na makuzi kwa watoto kwa lengo la kupata watoto wenye utimilifu wa akili.

Akifungua mafunzo hayo, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mwanahidi Ally Khamisi, alisema kutokana na umuhimu wa kukuza utimilifu wa akili ya mtoto, serikali itahakikisha inaendelea kutenga bajeti ili kutoa elimu kuanzia ngazi ya kijiji hadi taifa na kutokomeza hali hiyo.





# SMZ yajipanga udhibiti wa uingizwaji dawa za kulevya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harusi Said Suleiman, amesema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) imejipanga kukabiliana na uingizaji wa dawa za kulevya kwa kudhibiti bandari bubu ambazo hutumika kuziingiza dawa hizo.

Ofisini kwake jana, waziri huyo aliwaambia waandishi wa habari kuwa serikali kwa kushirikiana na vyombo vyake vya ulinzi katika maeneo ya mwambao, inatarajia kukitumia Kikosi cha Kuzuia Magendo Zanzibar (KMKM) kukabiliana na matukio ya uingizaji wa dawa za kulevya.

Alisema Zanzibar kuna zaidi ya bandari bubu 260 ambazo zote hutumiwa na wananchi kwa ajili ya kufanya shughuli za safari na kusafirisha bidhaa mbalimbali kwenda mikoa ya jirani ya Tanzania Bara.

Waziri huyo alisema Kisiwa cha Pemba pekee kinaongoza kwa kuwapo bandari bubu ambazo hutumiwa kwa safari zisizo rasmi kwenda mikoa jirani ya Tanzania Bara ikiwamo Tanga na Mombasa, Kenya.

"Katika kukabiliana na kupambana na uingizaji wa dawa za kulevya, tutakitumia zaidi kikosi chetu cha KMKM ambacho majukumu yake ni kulinda eneo la mwambao wa Pwani ya Unguja na Pemba," alisema.

Waziri huyo alisema dawa za kulevya ni janga la kitaifa ambalo waathirika wake wakubwa ni vijana kuanzia umri wa miaka 15 hadi 45 ambao ndiyo nguvukazi ya Taifa.

Mkuu wa KMKM, Azani Hassan Msingiri, alisema wamejipanga kukabiliana na uingizaji wa bidhaa kinyume cha sheria ikiwamo magendo ya bidhaa mbalimbali.

Alikiri ugumu wa kukabiliana na magendo katika Kisiwa cha Pemba kutokana na jiografia yake ya kuwapo bandari bubu nyingi ambazo siyo rasmi zinazotumiwa na wananchi na wavuvi kusafiri nje ya nchi.

"Kikosi cha KMKM tumejipanga kukabiliana na magendo na uingizaji wa bidhaa kwa kudhibiti bandari bubu ambazo ndiyo chanzo cha biashara ya dawa za kulevya," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Salama Mbarouk Khatib, alisema mchakato umeanza ikiwamo kurasimisha baadhi ya bandari zilizopo Pemba ili kila huduma ya usafirishaji iwe inafuata utaratibu halali.

Alisema kitendo cha kurasimisha bandari pia kwa kiasi kikubwa kitaiwezesha serikali kuingiza mapato yanayotokana na shughuli za usafirishaji na uingizaji wa bidhaa mbalimbali.

# Mwinyi aona fursa ushirikiano wa Afrika na China kibiashara

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amezikaribisha kampuni nyingi za China kuwekeza katika Bara la Afrika kwa kuwa kuna ardhi ya kutosha, nguvu kazi nyingi na Afrika ina uthubutu wa kufanya biashara.

Dk. Mwinyi alitoa rai hiyo wakati wa sherehe za ufunguzi wa mkutano wa tatu wa ushirikiano wa biashara kati ya China na Afrika uliofanyika katika Jiji la Changsha, Jimbo la Hunan, China.

Dk. Mwinyi alisifu ushirikiano baina ya China na Tanzania ambao sasa umetimiza miaka 60 huku kukiwa na matumaini utazidi kukua na kuimarika zaidi.

Alisema katika miaka miwili iliyopita, Afrika imeshuhudia ushirikiano mkubwa na China ambapo biashara imeongezeka kwa zaidi ya dola bilioni 74.

Alifurahi kuona wawekezaji wakubwa wa China wamehudhuria mkutano huo na akabainisha hiyo ni fursa kwa Afrika kujitutumua zaidi na kukaribisha wawekezaji hao barani.

Akifungua mkutano huo kwa niaba ya Afrika, Rais wa Malawi, Lazaro Chikwera, alitaka kuwe na mbinu madhubuti za kuzuia jaribio lolote la kupunguza kazi ya ushirikiano baina ya China na Afrika.

Rais Chikwera alisema China na Afrika hazina tena muda wa kuzorotesha uhusiano huo na kuwataka Waafrika kutumia kwa vitendo yale yote waliyojifunza kwa muda wote wa ushirikiano na China.

Aliwataka Waafrika kutumia kipindi hiki kutangaza zaidi bidhaa zao mbalimbali, akiomba China kufikiria kuanza kusamehe mikopo yake kwa Afrika ili kusaidia bara hilo kuendelea kupiga hatua kimaendeleo.



Mke wa Rais wa Zanzibar, Mama Mariam Mwinyi akielekea katika nafasi yake baada ya kumaliza kuzungumza katika mkutano wa Ushirikiano kati ya Wanawake wa Mataifa ya Afrika na China katika Jimbo la Hunan, China jana. **PICHA: IKULU**

# Tani 25 za dawa zateketezwa kisiwani Pemba

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

TANI 25 za dawa za binadamu zimeteketezwa kisiwani Pemba kufuatia msako uliofanywa na kubaini dawa hizo hazifai kwa matumizi ya binadamu. Ofisa Mwandamizi wa Wakala wa Dawa na Vipodozi Pemba, Nassir Salum, alisema jana kuwa dawa hizo zilinaswa kufuatia msako mkali uliofanywa na kitengo cha ukaguzi wa dawa na kuzibaini katika sehemu mbalimbali, yakiwamo maduka ya dawa.

Alisema dawa hizo zimepatikana katika maduka ya dawa yanayomilikiwa na watu binafsi, akikumbusja kuwa kuuza dawa zilizopita muda wa matumizi ni kosa la jinai.

Ofisa huyo aliwataka wamiliki wa maduka ya dawa za binadamu kufuata sheria zinazowataka kuhakikisha wanauza dawa zilizopo katika muda wake halisi. Alisema kitengo chao kinasisitiza na kuwataka wamiliki wa maduka ya dawa za binadamu kuhakikisha wanauza dawa zilizopo katika muda wake kwa ajili ya kulinda afya za binadamu.

Ofisa wa Idara ya Mazingira Pemba, Said Mbarouk, alisema kazi ya kuteketeza dawa zilizopita muda wake ilifanyika huko Kwale, Wilaya ya Pujini, Pemba kwa siku mbili.

Alisema tahadhari zote zilichukuliwa wakati wa uteketezaji wa dawa hizo, ikiwamo tahadhari za afya kutokana na hatari ya dawa kwa afya ya binadamu.

"Tumekamilisha kazi hiyo kwa siku mbili huko Kwale ambapo tahadhari zote za kiafya zimechukuliwa ili kulinda afya za binadamu," alisema.



ANJELINA

UKURASA 12

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE

JUMAMOSI JULAI 1, 2023



# WEMA LIA MAMA, USIKATE TAMAA

Mshindi wa mashindano ya Miss Tanzania mwaka 2006, mcheza filamu maarufu na mfanyabiashara, Wema Sepetu amejikuta akitokwa na machozi ya furaha, baada ya mashabiki wake wengi kumtumia meseji za faraja.

Hi ni baada ya staa huyo kusherehekea miaka miwili ya kuzaliwa kwa mtoto wa mpenzi wake wa sasa Whozu.

Whozu ambaye ni msanii mwimbaji alizaa na mpenzi wake wa zamani Tunda, lakini kwenye chapisho hilo la picha, Wema alisimama kama mama kwa mtoto huyo kusherehekea pamoja.

Mashabiki wengi mitandaoni walionekana kuvutiwa na jambo hilo kuwa la heri na hawakusita kumwandikia Wema jumbe za kumfariji kwa kukosa mtoto kwa muda mrefu, na kwa jinsi alivyoonesha mapenzi yake kwa mtoto huyo licha ya kwamba si mama yake mzazi.

Akitoa shukrani zake kwa meseji za faraja alizotumiwa, alizidiwa na hisia na kusema kuwa anawaza tu Mungu angezisikia dua zao na kumjibu ombi lake la kupata mtoto, kwani ana hamu sana kumpakata mwanawe siku moja.

"Sina lolote maskini ya Mungu ila nina furaha mwenzenu, unaweza kosa vingi ila Mungu akaamua tu kukufariji kwa namna yake, faraja hiyo ninayo ninayo Alhamdulillah... Mungu nitunzie hii faraja yangu, ibakiee tu " aliandika.

Katika mahojiano miezi michache iliyopita, Wema alitamka kuwa bado hajachoka kupambana kupata mtoto wake, licha ya kudanganywa na kuhadaiwa na wengi kuhusu dawa za kiasili ambazo hata hivyo hazijafua dafu kwa upande wake.


BASI SAWA

## Ustaa ulivyomfukuzisha shule Mr Blue

Mmoja wa waanzilishi wa muziki wa kizazi kipya Mr Blue amefunguka kuwa ustaa ndiyo uliomfanya aache shule, baada ya kutoa ngoma zilizokubalika ikiwemo 'Mapozi', iliyotoka zaidi ya miaka 10 iliyopita.

Staa huyo ambaye jina lake halisi ni Sameer Rajab amesema aliupata ustaa akiwa bado shule na kuwa bonge la tozi, hivyo hakuwa tayari kupigwa bakora mbele ya wanafunzi wenzake

"Kwakweli jambo lile lilinishinda sababu nilikuwa nimeshakuwa bonge la 'brazameni,' alafu niende shule kuchapwa bakora mbele ya wanafunzi alafu star, hicho ndicho kilichonifanya nisionekane tena yale maeneo na sikubahatika tena kurudi shule", alisema.



Alikuwa akielekeza sababu zilizomfanya shule kuona ngumu, alisema alitoa ngoma hizo akiwa shule na kupata shoo mbalimbali nchini Burundi ambako alikaa mwezi mzima.

Aliporejea akiwa ameweka na dawa kichwani, huku mitaani akiwa ameshakuwa supastaa, alipokea barua kutoka shule iliyomtaka kwenda kujibu mashtaka ya kutoonekana shule kiasi cha mwezi mzima. Hakwenda tena.

## Anjelina bado amlinda Harmonize

Mwimbaji wa muziki wa bongo fleva Anjelina George Kagusa maarufu kama Anjella amefichua kuwa kamwe hawezi kumsema vibaya Harmonize kwa kuvunja mkataba kwenye lebo ya Konde Music.

Anjella ambaye ana wiki moja na ushee toka aachie video ya Blessing, ikiwa ya kwanza toka atoke kwenye lebo hiyo alisema hawezi kusema ameonewa kwenye swala la Konde Music kuvunja mkataba na yeye kwa kuwa kilichosababisha mkataba uvunjwe kipo kwenye mkataba waliokubaliana kila upande.

"Mimi siwezi kusema kwamba wamenionea kwa sababu ishu ambayo ilisababisha kuvunjika ipo kwenye mkataba, hivyo ishu ya ugonjwa iko tofauti na haipo kwenye mkataba kwahiyo siwezi kusema kwamba nimeonewa", alisema Anjelina.





# MAMA KANUMBA BADO HAJAMALIZA

Mama wa mwigizaji filamu wa zamani, Steven Kanumba, Bi Flora Mutegoa, ameendelea kuelezea mlolongo wa matukio mabaya upande wake baada ya kifo cha mwanaye, akisema alitimuliwa kwenye nyumba akiwa kwenye msiba wa mwanaye kipenzi.

Hii si mara ya kwanza kwa mama huyo kudai kwamba alianza kuona maisha yanamuendea kombo baada ya kifo cha mwanawe 2012 jijini Dar es Salaam na kueleza mlolongo wa visa na mikasa vilivyomkuta.

Katika mahojiano mengine miezi kadhaa iliyopita, alisema kuwa alizuiliwa kabisa kutumia picha za mwanawe baada ya kifo chake, akisema kuwa hakuwa na hatimiliki kwa sababu mwanawe alikuwa anajitoa katika kila kitu kwa ajili ya  kuwafurahisha watu.

Sasa amekuja na hii mpya kuwa tukio ambalo lilitokea wakati wa msiba wa mwanawe na liliimuuma sana ni kutimuliwa kwenye nyumba ya kupanga wakati wa msiba wa mwanaye.

"Changamoto ni nyingi sana kwa mfano nilipata changamoto moja kubwa, sipendi kuiongelea lakini iliniumiza kimaisha. Mimi nilifukuzwa kwenye nyumba nikiwa kwenye msiba wa mwanangu lakini nilimwambia Mungu ahsante, nikawaza mwanangu angekuwepo hili tatizo lingeisha," alisema Bi Mutegoa.

## FILAMU

# Mdomo: Uliponza kichwa

**Na Adam Fungamwango**

KAMA ulivyo msemo huo, ndiyo hicho hicho kilichopo kwenye filamu hii iitwayo 'Mdomo.'

Ni filamu inayoonyesha jinsi mtu anavyoweza kuongea kitu kibaya kwa mtu mwingine, halafu baadaye kikamtokea na ingawa si yeye aliyesababisha, lakini kwa sababu alishawahi kuropoka, watu wanamhukumu kwa hilo.

Msemo huu wa 'mdomo uliponzwa kichwa', unafanana kabisa na ule anaosema 'aliwazalo mjinga ndilo linalomtokea.'

Imechezwa na wasanii Omari Mbwela, Yassin Kilungi, Wise Kidaba, Ijumaa Makwesa, Abdallah Ally, Arafa Abdallah, Viola Akilimali, Mwajuma Salum, Aisha Bakari, Shuda Lukenze, Evord Severini, Queen Geofrey na wengineo.

Inaanza kwa kuonyesha ujirani wa wakazi wawili wa kijiji fulani nchini, Mapui na mwenzake Mbwela.

Kila mmoja ana shamba lake, lakini la Mbwela lipo mbele zaidi ya Mapoi, hivyo wakitaka kulima ni lazima kwanza Mapoi asubiri kwanza Mbwela apitishe trekta kwenye shamba la mwenzake likalime kwake, akimaliza ndipo Mapoi naye alime. Ni kwa sababu njia ya kupita trekta inapita shambani kwake kwanza.

Mwaka huo haikufanyika hivyo. Mapoi alilima kabla mwenzake hajapitisha trekta, Mbwela alivyoona hivyo hivyo na yeye akapitisha trekta kwenye shamba na mwenzake, mazao yote yakakanyagwa.

Ugomvi ukaanza kila mmoja akimuona mwenzake ni mkosefu. Ukaenda mbali zaidi mpaka kutishiana maisha na kuuana kwa uchawi.

Kila mtu akarudi nyumbani kwake. Baada ya siku chache kila mmoja akaanza kuumwa. Waliumwa na kila mmoja akawa anamtuhumu mwenzake kuwa amemroga.

Ndugu wa pande mbili wakawa wanapishana na waganga na hospitali kusaka tiba za ndugu zao, lakini wapi.

Kila mmoja akaenda kwa Mwenyekiti wa Kijiji kwenda kushtaki ndugu yao walivyorogwa na mwenzake.

Hata hivyo, hakuna ndugu wa upande wowote aliyekuwa anajua, upande wanaoutuhumu nao kuna mgonjwa.

Kila upande ulijua wa kwao ndiyo anaumwa pekee. Mwenyekiti wa Kijiji alibaini hilo baada ya wote kwenda kushtaki kwa nyakati tofauti.

Hali za Mapoi na Mbwela zikawa mbaya kiasi kwamba ndugu za pande zote mbili wakachukua panga ili kwenda kulipizana kisasi. Wakakutana njiani. Ukawa ugomvi. Kabla hawajaanza kupigana, akajitokza mzee mmoja jirani akaitwa Kopoka. Akawaambia hakuna yoyote kati ya hao aliyemroga mwenzake. Akasema yeye ndiye aliyewaroga wote wawili baada ya kusikia wanazozana kuhusu masuala ya shamba. Na alifanya hivyo kwa nia ya kuwashikisha adabu kuwa siku nyingine wasipende kuogea vitu ambavyo hawaviwezi kwa sababu mdomo uliponza kichwa. Atawapa dawa, wote wawili wakapona na kurejea kwenye hali ya kawaida.







# Meja Kunta ana tabia mbaya

Mkali ya muziki wa singeli, Meja Kunta amekiri kuwa ana tabia mbaya, huku akiomba Mungu mtoto wake aliyenaye na atakaowapata baadaye wasirithi tabia yake hiyo.

Meja kasema haelewi kwa nini, lakini amekuwa hapendi kuwa na mahusiano na mtu kwa muda mrefu, huwa inamchosha sana, na hiyo ameieleza kuwa ni tabia yake mbaya, anajua kuwa ni mbaya, lakini hawezi kuiacha.

"Nina tabia mbaya nyingi, lakini sipendi mtoto wangu niliyenaye na hata wanangu watakaokuja wasije kurithi.

Kwanza kabisa nimekuwa sipendi mahusiano ya muda mrefu, nachukia sana mahusiano, siwezi kudumu na mtu muda mrefu, hiyo ni tabia yangu yaani, nimekuwa tu na hulka hiyo, yaani kukaa na mpenzi muda mrefu nachoka aaa, naona aaa, napenda mwanangu, aje aolewe mapema kwa sababu ni mtoto wa kike, napenda adumu na mumewe, lakini mimi baba yake du, hatari sana. Hata nikipata wa kiume napenda awe na mpenzi mmoja na hata akioa adumu naye," alisema msanii huyo.

# WASANII, WANAMUZIKI NDUGU BONGO

**Na Adam Fungamwango**

KWA asilimia kubwa kipaji huwa hakirithishwi. Kipaji ni uwezo na karama inayotoka kwa Mungu kwenda kwa binadamu mmoja pekee. Hata hivyo mara chache hutokea, watoto kurithi vipaji vya baba zao. Hata hivyo ni lazima kutakuwa na utofauti. Mmoja wapo, baba au mtoto atakuwa juu kuliko mwenzake.

Pia hutokea mara chache ndugu wa kuzaliwa kuwa na kipaji cha aina moja. Wanaweza kuwa waigizaji, wanamuziki, wachoraji, au wanamichezo.

Mfano kwenye soka nchini Tanzania kuna Mbwana Samatta na ndugu yake Mohamed Samatta. Huko nyuma kulikuwa na ukoo wa kina Kihwelo. Mussa Kihwelo, Mwesa Kihwelo, Mtwa Kihwelo, Jamhuri Kihwelo, Muhehe Kihwelo na wengine, wote hao wakiwa ni wacheza soka.

Kulikuwa na Kitwana Manara, Sunday Manara na Kassim Manara. Kwa upande wa muziki hasa wa nje ya nchi kwa vijana wa sasa kuna mapacha waliounda kundi la P-Square ambao ni Peter Okoye na Paul Okoye.

Hapa Tanzania wanandugu ambao wamekuwa na vipaji vya muziki na kuwa maarufu sana tangu enzi za miaka ya '70 mpaka sasa.

**Familia ya kina Uvuruge**

Kama Tanzania imewahi kupata wanamuziki wengi kutoka kwenye familia moja kama ilivyokuwa kina Kihwelo kwenye soka, basi ni ukoo wa kina Uvuruge.

Ni familia maarufu sana kwenye muziki wa dansi tangu miaka ya '70. Hao ni kina Jumanne Uvuruge, Khalfan Uvuruge, Uruka Uvuruge, Maneno Uvuruge na Fadhili Uvuruge.

Ni wanamuziki wa familia ya wanamuziki wakubwa kabisa nchini, waliopata heshima kwa uwezo mkubwa wa kupigia bendi mbalimbali nchini.

Jumanne ndiye mtunzi wa wimbo maarufu sana nchini wa Safari Trippers 'Georgina' ambao hakuna  'live' yoyote ya bendi itamaliza muziki bila kupiga wimbo huo.

**Ali Kiba na Abdul Kiba**

Naweza kusema kuwa familia hii imebarikiwa, kwani pamoja na kwamba wote wawili wana uwezo mkubwa wa kucheza soka na ushuhuda watu huwa wanajionea kwenye tamasha la 'team Kiba na team Samatta' , lakini wote pia ni wasanii maarufu wa muziki wa bongo fleva.

Ali na Abdul kila mmoja anafanya kazi kivyake, kila mtu akitoa ngoma yake kwa wakati wake, na wamekuwa wakilitikisa soko la muziki wa kizazi kipya.

**Ezekiel Mazanda na David Mazanda**

Hawa ni wanamuziki waliokuwa mapacha.  Wote walikuwa wanapiga gitaa la kati 'rhythm'.

Waliwika sana mwanzoni mwa miaka ya '80 walikuwa kwenye bendi mbili tofauti.

Ezekiel, alikuwa ni mwanamiziki wa bendi ya Urafiki Jazz, huku pacha mwenzake David akiwa ni mwanamuziki za bendi ya Bima Lee. Wote wamefariki dunia kwa nyakato tofauti.

**Wilson Peter na George Peter**

Ni wanamuziki ndugu ambao ni maarufu zaidi kwenye muziki wa dansi si Tanzania tu, bali Afrika Mashariki. Vijana hawa Watanzania kutoka Hale mkoani Tanga, walikuwa wanamuziki wa Jamhuri Jazz Band, kabla ya kujiengua na kuunda bendi ya Arusha Jazz, baadaye ikavuka mpaka na kuingia nchini Kenya ambako waliibadilisha jina la kuiita Simba Wanyika.


Wilson ambaye ni mkubwa, yeye ndiye alikuwa kiongozi, akipiga gita la solo, akiimba sauti ya kwanza, huku mdogo wake George ambaye aliimba sauti ya pili na ya tatu, sauti ambayo iliigwa na Tx Moshi William baadaye.

Wakati Geogre akifariki mwaka 1992, kaka yake Wilson alifariki mwaka 1995, wote wakizikwa nchini Kenya.

**James Kibosho na Martin Kibosho**

Akina Kibosho ni wapiga drums maarufu sana nchini, wakiwa wamepitia bendi mbalimbali kama vile Extra Bongo, Twanga Pepeta na bendi mbalimbali za muziki wa dansi wa kisasa.

James na Martin Kibosho ambao ni mtu na mdogo wake, ni moja kati ya familia chache nchini ambazo zimetoa ndugu wenye kipaji cha aina moja na hadi leo wanaendelea na muziki kwenye bendi mbalimbali nchini.





# Yvonne,Sarkodie hapatoshi

MAJIBIZANO makali yanaendelea kati ya mwigizaji wa Ghana, Yvonne Nelson na rapa Sarkodie, ambayo yamejikita nani aliyesababisha mrembo huyo kuamua kutoa ujauzito.

Yvonne katika kitabu chake ameeleza jinsi mwanamuziki huyo alivyoshindwa kuwajibika pale alipompa ujauzito na kusababisha kuchukua hatua ya kuutoa.

Mwigizaji huyo alifichua hayo katika kitabu chake kinachoitwa 'I Am Not Yvonne Nelson' kilichozinduliwa Jumapili, Juni 18, 2023.

"Sikuwa mimi pekee niliyehusika na hali hiyo, kwa hivyo nilimwita mtu ambaye mbegu yake yenye nguvu ilikuwa imekuwa ndani yangu jina lake ni Michael Owusu Addo, mwanamuziki mashuhuri wa Ghana ambaye anajulikana zaidi kama Sarkodie," alisema.

Lakini Sarkodie akijibu tuhuma hizo katika wimbo wake mpya, 'Try Me ' uliotolewa juzi alidai alimwomba Yvonne Nelson kubaki na ujauzito huo ingawa hakuwa tayari kuwa baba.



## Ni Kanye West tena

KILA kukicha ni heri ya jana! Ndiyo hali inayomkuta rapa maarufu wa Marekani Kanye West, ambaye kila siku ni mtu wa majanga na hivi sasa anakabiliana na tuhuma nzito ya kumdhulumu mshikaji wake.

Alex Klein, mjasiriamali wa teknolojia ambaye alifanya kazi na rapa huyo ambaye walikuja kutengana baada ya West kumsifu Hitler hadharani na kusababisha kutupiwa lawama ulimwenguni kote.

"Tulikataa dola milioni 10. Kanye alikasirika sana," amesema Klein katika kipindi cha BBC The Trouble with Kanye.

Kulingana na Klein, ambaye alifanya kazi na West kati ya 2019 na 2022, matamshi yake ya hadharani ya chuki ni mkakati wa kisiasa na wa makusudi kudhulumu haki yake.

## Blackface hatakagi usumbufu

KATIKA kile kinachoonekana kama kutoisumbua mahakama, Rapa Blueface amekiri mashtaka ya kutoa bunduki kwenye gari la mtu, na kuondoa betri.

Blueface atawasilisha ombi lake rasmi Julai 3, mwendesha mashtaka Nick Portz alithibitisha hilo na amesema jimbo la Nevada halitapinga hukumu ya majaribio wakati ombi hilo litakapowasilishwa rasmi.

Kulingana na hati za kisheria zilizopatikana na TMZ, Blueface alikuwa katika Klabu ya Euphoric Gentlemen's huko Las Vegas mnamo Oktoba 2022, wakati mtu anayedaiwa kumpiga risasi alionekana kufanya mzaha akimwambia huyo anazungumza na wanawake katika gari bovu.





## Dr Dre kupewa hadhi Hollywood

Wasanii maarufu nchini Marekani Dr. Dre na Angie Martinez ni miongoni mwa waburudishaji 31 ambao wamechaguliwa tuzo ya Hollywood Walk of Fame.

Kamati rasmi ya uteuzi ya Walk of Fame iliyojumuisha washindi wa zamani wa Walk of Fame ilitangaza washindi wapya katika mkutano na waandishi wa habari.

Ellen K, mtangazaji maarufu wa redio ya KOST na mwenyekiti wa kamati ya uteuzi ya Walk of Fame, alitangaza majina ya watu hao maarufu ambayo yatawekwa katika alama ya nyota.

"Kamati ilifanya kazi ya kubwa kuchagua watu hawa wenye talanta," alisema.

## Nicki Minaji kumbe ana utu

Rapa Nicki Minaj anaonekana kuwa na moyo wa utu baada kusaidia gharama za masomo kwa kijana wa Chicago mwenye umri wa miaka 14 ambaye alikamatwa na mama yake, Carlishia Hood, baada ya tukio la kupigwa risasi wiki kadhaa nyuma.

Hivi majuzi video iliibuka mtandaoni baada ya Hood akionekana akishambuliwa vikali na mwanamume anayeitwa Jeremy Brown wakati wa mabishano makali na kisha alimpiga risasi na kumuua .

Inasemekana alichukua hatua hiyo katika juhudi za kumlinda mama yake.







Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Emigidius Kasunzu (kulia) akikabidhi rasmi ofisi hiyo kwa Mkurugenzi Mtendaji mpya wa Halmashauri hiyo, Dk. Jumaa Mhina wilayani humo juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Mapato 'kiduchu' yamshitua RC

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MAPATO 'kiduchu' yanayokusanywa katika Halmashauri Wilaya ya Monduli tofauti na makisio ya makusanyo ya ndani, yamemshtua Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella.

Kiongozi huyo pia ameshtukia kuwapo mchezo mchafu wa baadhi ya wanaokusanya mapato, kuchezea mfumo wa ukusanyaji mapato.

Mongella alieleza kushtushwa kwake na hali hiyo jana wakati wa kikao maalum cha Baraza la Madiwani kilichojadili utekelezaji wa taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu na Serikali za Mitaa (LAAC).

"Mkurugenzi hali ya ukusanyaji wa mapato siyo mzuri katika Halmashauri ya Monduli. Lakini pia kuna mchezo wa kuchezea mfumo wa ukusanyaji mapato.

"Hali hii ndiyo inayosababisha hata vikao vya halmashauri kutofanyika kwa miezi mitatu, huku kukiwa na madeni ya posho za vikao," alisema.

Kutokana na hali hiyo, Mongella alimwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Monduli, Happyness Laizer, kusimamia kikamilifu ukusanyaji wa mapato kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo badala ya kutegemea ruzuku za serikali kuu.

"Haiwezekani mtegemee ruzuku za kutoka serikali kuu wakati huku mnachezea mfumo wa ukusanyaji mapato," alionya.

Mongella pia aliagiza kila Diwani asimamie miradi kikamilifu iliyoko katika kata yake kwa kuwa miradi hiyo siyo ya halmashauri wala mkuu wa mkoa.

Kuhusu malalamiko ya Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Issac Copriano, maarufu Kadogoo, kutokubali kikao hicho kiendelee kwa madai kuwa amewekewa makabrasha mezani asubuhi, yeye na madiwani wake, Mongella alikiri kuyapokea.

"Malalamiko yako Kadogoo nimeyapokea na nimekuelewa vizuri. Ninakuomba uwe na amani, lakini pia ninakuomba uridhie kikao kianze tupitie hoja za CAG, kwa sababu ni wajibu wetu kuhakikisha Monduli inasonga mbele kwa sababu ni wilaya yenye historia ya kipekee," alisema.

Awali Kadogoo alisema hayuko tayari kuruhusu kikao hicho kiendelee kwa sababu hana uelewa wowote wa ajenda zitakazojadiliwa na madiwani wake kwa kuwa makabrasha ya vikao aliwekewa mezani asubuhi.

"Siko tayari kuendesha kikao ambacho ajenda zake sijazipitia, wala sizifahamu maana nilipewa taarifa za kikao kupitia simu ya kiganjani.

"Kibaya zaidi, nilimwita mkurugenzi asubuhi hii ili tujadili hizi ajenda akakaidi. Nikamtuma Ofisa Utumishi, Jenifer Mapembe, amwite akakaidi. Mkuu wa Wilaya akamwita akasema anakwenda hospitalini, lakini cha ajabu sasa hivi ameingia kwenye kikao.

"Sisi Wamasai hatupendi dharau dharau. Ni bora nikaukosa udiwani na Uenyekiti wa Halmashauri kuliko kudharauliwa.

"Na kama nina upungufu, ninaomba niambiwe upungufu wangu, lakini siyo kudharauliwa. Nilikuwa mwenyekiti wa kipekee, ambaye ninatetea sana maslahi ya watumishi lakini sasa itabidi nibalike," alisema.

## Halmashauri yashindwa kuzijibu hoja 19 za CAG

**Na Mary Mosha,** MOSHI

HALMASHAURI ya Wilaya Moshi mkoani Kilimanjaro haijajibu hoja 19 kati ya 33 zilizoko katika taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) za mwaka wa fedha 2021/22.

Hayo yalibainishwa jana katika taarifa iliyowasilishwa na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Amir Nyawaya, katika kikao maalum cha Baraza la Madiwani kilichofanyika kwa lengo la kujadili utekelezaji wa hoja za CAG na maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu na Serikali za Mitaa (LAAC).

"Baada ya uhakiki wa majibu ya hoja za ukaguzi na utekelezaji wake uliofanyika mwezi Mei 2023, hali ya hoja za ukaguzi inaonyesha mwaka 2019/20 hadi 2020/21 kulikuwa na hoja 12, hoja zilizofungwa tatu na hoja ambazo hazijafungwa ziko tisa.

"Na katika mwaka wa fedha 2021/22 kulikuwa na idadi ya hoja 21, hoja zilizofungwa mpaka sasa ni 11 na hoja 10 hazijafungwa," alifafanua.

Kutokana na hali hiyo, Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro, Tixon Nzunda, alisema halmashauri hiyo inaongoza halmashauri zote saba za mkoa huo kupata hoja nyingi za CAG.

"Jielekekezi kujiimarisha zaidi katika mifumo ya ndani ya halmashauri na kutoa majibu ya hoja zote zilizotolewa na CAG mapema ili hoja hizo zifungwe," aliagiza.

Awali Mkaguzi wa Nje wa Hesabu za Serikali Mkoa wa Kilimanjaro, Anold Kishimbo, alisema kasi ya ufuatiliaji wa menejimenti kuhusu mapendekezo ya CAG ni ndogo, akiwataka kuongeza kasi ili hoja hizo zisikutwe katika mwaka mwingine wa fedha.

# Utafiti mpya wabaini mbinu kuukabili uhaba wa walimu

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

RIPOTI mpya ya utafiti wa Vodacom Group, Vodacom, Safaricom na Taasisi ya Nelson Mandela Foundation inaonyesha nyenzo za kidigitali na teknolojia, zina nafasi kubwa zaidi ya kutoa suluhisho la haraka na kwa gharama nafuu katika kutatua tatizo la uhaba wa walimu.

Imeelezwa kuwa teknolojia za kidijitali zinaweza kuwaunganisha walimu na wanafunzi walioko mbali na jamii, pia katika maboresho ya mifumo ya elimu ya kiafrika.

Mkurugenzi Mkuu wa Vodacom Group, Shameel Joosub, akizungumza jana wakati wa kuwasilisha ripoti hiyo, alisema utafiti huo unaonyesha kuwapo ongezeko kubwa la upatikanaji wa elimu barani Afrika, isipokuwa kuongezeka kwa upatikanaji wake haimaanishi ukuaji wa ubora wa elimu inayotolewa.

Alisema kukiwa na unafuu na uhakika wa uunganishwaji, nyenzo za kidigitali na teknolojia zinatoa suluhisho kwa gharama nafuu. Alisema kuwa ili kukabiliana na tatizo hilo, maboresho yaliyopendekezwa na ripoti hiyo, yatawawezesha vijana kuunganishwa na wakufunzi wenye ujuzi wa hali ya juu na kuwasaidia kuyatumia masomo wanayojifunza kuwa maarifa yenye manufaa kwao.

"Tumeshuhudia hili kupitia miradi na programu zetu za elimu tunazoziendesha, zikilenga upatikanaji wa nyenzo za elimu bora, kuwezesha mtu kujifunza popote alipo. "Na namna bora ya elimu kwa walimu na wanafunzi kwa sehemu ya jamii za kiafrika ambazo zina rasilimali pungufu." alisema Joosub.

Aliongeza kuwa taarifa ya utafiti inaangalia hali ya elimu barani Afrika kwa sasa, ikionyesha namna teknolojia za kidigitali na uunganishwaji, zikijumuishwa na mifumo thabiti, kuungwa mkono na serikali na wadau tofauti katika sekta, zinavyoweza kutumika kupunguza vikwazo vya elimu barani.

Kwa mujibu wa Joosub, hiyo ni sehemu ya mpango wa uunganishwaji wa shule kwa kushirikiana na taasisi ya African Child Projects na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF), ambao unalenga kuzifikia shule 300 za umma nchini kote katika awamu ya pili.

Alibainisha kuwa mpaka sasa wanafunzi 600,000 wamenufaika na mpango wa uunganishwaji wa shule nchini.

Katika hafla hiyo, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Nelson Mandela Foundation, Prof. Verne Harris, alisema "upatikanaji wa elimu bora ni muhimu katika mapambano dhidi ya umasikini unaoweza kurithishwa kutoka kizazi kimoja kwenda kingine ikiwamo kuleta usawa.

"Taasisi ya Nelson Mandela siku zote inasisitiza namna gani elimu ni muhimu, sio kwa kujitambua pekee bali pia kwa kuleta mabadiliko ya mtu binafsi na kubabidili mwelekeo wa jamii kuwa na usawa, haki na utu," alisema.

Mtaalamu wa elimu mashuhuri wa kimataifa na miongoni mwa waandishi wa ripoti hiyo ya utafiti, Prof. Jonathan Jansen, alisema "vikwazo hivi vinahusisha kila kitu kuanzia ukosefu wa nishati ya uhakika ya umeme, msaada wa uhakika wa kiufundi na upungufu wa upatikanaji wa intaneti mpaka vikwazo vya lugha, kutokuwapo kwa utulivu wa kisiasa na vikwazo vya kijamii.

"Lakini kwa sera sahihi, miundombinu na utayari katika uwekezaji, maboresho ya kidigitali yanaweza kutoa fursa kwa vijana wa Afrika, kufurahia mustakabali wenye usawa, endelevu, na ulioiunganishwa," alisema.

MAKALA

## TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Msemo 'nyama ya ulimi' ulianzia hapa

**Na Adam Fungamwango**

HUKO nyuma tuliwahi kuweka hadithi ya mapokezi 'ulimi uliponza kichwa', ambao ulianzisha misemo ya 'utakiona cha mtema kuni, inayotumiwa hadi kwenye kizazi cha sasa.

Tuliona jinsi mtu mmoja anayejishughulisha na kazi ya kukata kuni akiitwa 'mtema kuni' alipokwenda porini siku moja kusaka kuni za kuja kuuza kijijini, lakini alikutana na mti ambao alipotaka kuukata ukamuomba msamaha, lakini ukawa unasema 'ulimi uliponza kichwa.'

Ilikuwa ni ajabu kwa 'mtema kuni', hivyo akarejea kijijini na kuwaambia watu vimbwanga alivyovipata akiwa porini siku hiyo.

Habari hiyo pia ikamfikia mfalme, akamwita 'mtema kuni' ambaye maana yake ni 'mkata kuni', na kumuuliza kama habari hizo ni sahihi? Alipojibu ndiyo, mfalme akamuonya kuwa yeye hasumbuliwi, akikuta vinginevyo amfanye nini? Kwa kujiamini akasema akatwe kichwa.

Walipofika porini kwenye mti ule haukuongea. Siku nzima walishinda hapo, lakini wapi. Mfalme akaamuru 'mtema kuni' akatwe kichwa mara moja. Walinzi walipotekeleza agizo lile, kiwiliwili kilipotenganishwa na kichwa, mti ulianza kuongea maneno yale yale aliyoyasikia marehemu siku hiyo, 'ulimi uliponza kichwa.' Licha ya mfalme na watu wote kusikitika, lakini jamaa alikuwa tayari ameshauawa. Ndipo msemo 'ulimi uliponzwa kichwa' na 'utakiona cha mtema kuni', ulipozaliwa.



Malkia

Leo tutaangalia hadithi nyingine ya mapokeo, iliyozaa msemo wa 'nyama ya ulimi.' Ni hadithi inayomhusu mfalme wa himaya moja na masikini.

Aliishi mfalme mmoja kwenye nchi moja, lakini kwenye himaya yake pembeni ya mji aliishi masikini, aliyekuwa anapata riziki yake kwa kwenda mjini kufanya vibarua vya kulipwa kwa siku na kurejea kwenye kijumba chake kibovu.

Mfalme alikuwa na mkewe, ambaye hakuwa na siha nzuri, lakini alionekana mrembo kwa sababu ya kujipamba na vito vya thamani na dhahabu.

Mke wa masikini hakuonekana mrembo kwa macho ya kawaida, lakini alionekana kuwa na siha nzuri. Walinzi wa mfalme walipita siku moja na kumshangaa mke wa masikini alivyokuwa ana siha njema.

Wakaenda kumwambia mfalme ambaye naye alipokuja kuthibitisha, alimwambia masikini wabadilishane. Masikini akawa na mashaka, akimwambia mke wa mfalme hawezi kuishi kwenye kijumba kibovu na kula chakula anachokula yeye. Neno la mfalme ni amri, mwisho wa siku wakabadilishana.

Mke wa masikini alivyochukuliwa na mfalme alifika kwenye himaya na kuanza kusimangwa kwa maneno mbalimbali ya 'kula chakula ambacho hujawahi kukila tangu kuzaliwa.' Maneno ya masimango, kashfa na majigambo ya mfalme yalimfanya mwanamke aishi kinyonge, akakonda baada ya mwezi tu na siha yote ikapotea.

Masikini ambaye alimchukua mke wa mfalme aliondoka asubuhi kuhemea akimpa maneno matamu na ya faraja mwanamke ambayo hajawahi kuyasikia popote pale. Mwezi mmoja baadaye pamoja na shida zote, akanenepa na kuwa mzuri zaidi ya alivyokuwa kwa mfalme, licha ya mavazi duni.

Mfalme kuona hivyo alimfuata masikini na kumuuliza ni chakula gani anachowalisha hawa wanawake? Akajibiwa ni nyama ya ulimi.

Mfalme akamchukua kwa nguvu mkewe wa zamani aliyempa masikini, na yeye akamuachia wa kwake aliyemchukua.

Akapiga marufuku wauza mabucha wote kwenye himaya yake kumuuzia nyama ya ulimi masikini, badala yake wapeleke kwake tu.

Akawa na kazi ya kumlisha mkewe nyama ya ulimi, akimlazimisha hata kama ameshiba. Mke akakumbusha wema na faraja aliyokuwa akiipata kwa masikini. Mwezi tu akakonda hata ukimtupia mbwa hamli.

Mke wa masikini alirudi kwenye hali yake ya zamani. Akanawiri kuliko mwanzo. Hii ilimuuma mfalme. Akaamuaru wauza mabucha wote wakamatwe kwa madai wanamuuzia masikini nyama ya ulimi kinyemela.

Halafu akaamuru masikini na mkewe waletwe mbele yake. Akawaita wauaji wake wakiwa na majambia. "Haya niambie, ni kitu gani unachofanya kinasababisha hawa wanawake wanawiri na kuwa na furaha. Awali ulinidanganya kuwa nyama ya ulimi, nimefanya hivyo lakini sikupata matokeo mazuri, leo niambie ukweli, sivyo nakukata kichwa." Akang'aka mfalme.

"Samahani mtukufu mfalme, nilivyosema nyama ya ulimi sikumaanisha nyama hii ya buchani. Ila ni maneno mazuri ya furaha na faraja. Mwanamke anataka apendwe, abembelezwe, asikilizwe, adekezwe hata kama una hali duni vipi, ataishi kwa furaha na amani na kunawiri." Masikini akamjibu kwa unyeyekevu.

Ndipo akili ya mfalme ilipofunguka. Akaamuru kuachiwa kwa wauza bucha wote, akamsimika masikini kuwa Waziri Mkuu kutokana na hekima na busara zake akiona zitamsaidia kwenye majukumu yake. Hapo ndipo msamiati 'nyama ya ulimi' lilipozaliwa, ikiwa na maana ni 'maneno matamu.'

**Tuma meseji 0716 350534**



Masikini



Mfalme

## WFP yasaidia vifaa vya TEHAMA wizarani

Na Faustine Feliciane

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Chakula (WFP) limeikabidhi Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi vifaa vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) vyenye thamani ya Sh. milioni 44.

Vifaa hivyo vinajumuisha kompyuta, printa na mashine ya kudurusu ambavyo vimekabidhiwa katika ofisi ndogo ya wizara iliyopo jijini Dar es Salaam.

Mkurugenzi na Mwakilishi Mkazi wa WFP, Sarah Gordon-Gibson alikabidhi vifaa hiyo jana na kupokewa na Mkurugenzi wa Huduma za Wakimbizi wa Wizara, Sudi Mwakibasi kwa niaba ya serikali.

Akizungumza mara baada ya kuvipokea, Mwakibasi alisema vifaa hivyo vitatumika katika idara anayoisimamia . Vitaongeza ufanisi, hasa wa TEHAMA.

"Tunawashukuru WFP kwa utekelezaji wa maombi yetu, vifaa hivi tulikuwa tunavihitaji sana kwa ajili ya kuongeza ufanisi katika idara yetu," alisema Mwakibasi.

Alisema shirika hilo limekuwa mshirika mzuri wa serikali ambapo mbali na kutoa chakula kwa wakimbizi waliopo kambini nchini, wamekuwa wanafanya mambo mengine ya ziada na kuisaidia serikali.

"Kule katika kambi za wakimbizi kumekuwa na amani kwa sababu ya uhakika wa chakula kutoka WFP, lakini wamekwenda mbali zaidi, kwa sasa wanatoa elimu ya matumizi bora ya ardhi kwa wakimbizi," alisema.

Mwakibasi alisema kutokana na elimu hiyo, wakimbizi saa wamekuwa wakizalisha chakula.

Mkurugenzi wa WFP, Sara alisema wataendelea kushirikiana na Tanzania katika kuhakikisha wakimbizi wanakaa kwa amani na kupata mahitaji yao muhimu.

"Tumekuwa na programu nyingi za kusaidia wakimbizi, tutaendelea kufanya kazi kwa karibu na Tanzania, vifaa hivi tulivyokabidhi leo (jana) tunaamini vitasaidia katika utendaji kazi wa wizara hii kuwahudumia wakimbizi waliopo hapa Tanzania," alisema Sarah.

# Wanawake walivyotikisa mitihani ya CPA

Na Joseph Mwendapole

MATOKEO ya mitihani ya Shahada ya Juu ya Uhasibu (CPA), yanaonyesha wanawake wameongoza kwa idadi kubwa kulinganisha na wanaume waliofaulu mitihani hiyo.

Matokeo hayo yalitangazwa jana na Mwenyekiti wa Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA), Prof. Sylvia Temu. Waliofaulu ni 394.

Alisema matokeo hayo yaliidhinishwa hivi karibuni na bodi ya wakurugenzi iliyoketi Juni 27. Kati ya watahiniwa 394 waliofaulu, wanawake ni 199 sawa na asilimia 50.5 na wanaume ni 195 sawa na asilimia 49.5.

Alisema idadi hiyo inafanya jumla ya watahiniwa waliofaulu mitihani ya CPA kufikia 12,547 tangu mitihani hiyo ianze nchini mwaka 1975.

Mwenyekiti huyo alisema mitihani hiyo ilifanyika katika vituo 12 vya mitihani vilivyopo Tanzania Bara na Zanzibar. Ilihusisha watahiniwa katika hatua ya kwanza na ya pili katika ngazi ya cheti cha utunzaji wa hesabu.

Alitaja hatua hizo kuwa ni ATEC 1 na ATEC 11 zenye masomo manne kila moja na ngazi ya taaluma. Alisema kati ya watahiniwa 394 waliofuzu na kutunukiwa cheti cha Taaluma ya Juu ya Uhasibu (CPA T) wengi wao wametoka vyuo mbalimbali. Watahiniwa 89 walitoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM). Prof. Temu alisema watahiniwa 68 wanatoka Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IMF), 66 walitoka Chuo Kikuu Mzumbe, 50 wametoka Chuo cha Uhasibu Tanzania na 18 wametoka Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM).

Alisema jumla ya watahiniwa waliosajiliwa ni 6,837 wakati 505 hawakufanya mitihani hiyo kutokana na sababu mbalimbali. Kati ya watahiniwa wote waliofanya mitihani, wanawake ni 3,112 na wanaume ni 3,220.

Prof. Temu alisema kwa upande wa cheti cha utunzaji wa hesabu (ATEC), watahiniwa 43 wamefaulu mtihani wa ngazi hiyo na idadi hiyo inafanya jumla ya watahiniwa waliofaulu mitihani hiyo tangu kuanzishwa kwake mwaka 1991 kufikia 4,285.

Aliwapongeza waliofaulu vizuri mitihani yao na kuwataka ambao hawajafuzu, wasikate tamaa. Waongeze bidii zaidi katika masomo yao ili wafanye vizuri zaidi katika mitihani ijayo ya bodi.

Aliwashauri kutumia vyema vitabu vilivyotayarishwa na bodi katika kujiandaa kwa mitihani yao na kusoma vitabu vingine vya ziada ili kuongeza ufahamu zaidi katika masomo yao.

Kiongozi huyo pia alisema NBAA inaendelea kuboresha mitaala yake ya masomo. Itaanza kutumika kuanzia muhula wa mitihani wa Novemba 2024.



Mwanafunzi wa kidato cha nne Shule ya Sekondari Kerezange, jijini Dar es Salaam, Jacqueline Jairo, akichangia hoja kwenye kikao cha bunge la wananchi lililoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Kivule jana, kwa ajili ya kujadili bajeti kuu ya serikali kama imezingatia mrengo wa kijinsia. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Kamishna wa madini aita wawekezaji madini na vito

Na Christina Mwakangale

KAMISHNA wa Madini, Abdulrahman Mwanga, amewakaribisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuwekeza nchini, hususan katika kuongeza mnyororo wa thamani wa madini na vito.

Mkoani Dar es Salaam jana, Mwanga alitembelea Banda la Madini, akimwakilisha Katibu Mkuu Wizara wa Madini, Kheri Mahimbali, katika Maonesho ya 47 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (DITF).

Alisema Tanzania inafanya vizuri katika uwekezaji hususan eneo la utafiti na uchimbaji wa madini, ingawa katika kuyachakata na kuwa tayari kwa kuuzwa. "Tumefanya vizuri sana katika uwekezaji, hasa katika uchimbaji na kufanya utafiti. Sekta ya Madini ni muhimu na inachangia kwa asilimia 50 katika fedha za kigeni nchini, hivyo fursa za uwekezaji zipo, tunawakaribisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi," alisema Mwanga.

Alimtaka kila Mtanzania achangamkie fursa ya uwekezaji kupitia sekta hiyo, ikiwamo katika viwanda vidogo vya madini kwa kuwa kuna mahitaji ya huduma tofauti kama vile chakula, malazi na elimu. Mkurugenzi Mwenza wa Kampuni ya TanzaKwanza, Francis Mlacha, alisema kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade), wameandaa kituo kimoja cha kuonyesha bidhaa zitokanazo na madini.

"Lengo la kuwa na kituo kimoja katika Banda la Madini ni kuwapa unafuu watembeleaji kwenye maonesho haya, kupata huduma ya sekta hii kwenye kituo hiki. Pia kuhakikisha maonesho haya hayaishii kuonesha bali kunakuwa na jukwaa la biashara la madini.

"Matarajio ni kukutanisha wafanyabiashara wa nchini na soko la nje, ili kuongeza fursa kwa wafanyabiashara sekta hii," alisema Mlacha.

# India yaombwa kushiriki kukuza uchumi wa bluu

Na Halfani Chusi

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano Afrika Mashariki, Balozi Dk. Samwel Shelukindo, ameiomba Serikali ya India ishirikiane na Tanzania kukuza sekta ya uchumi wa bluu ambayo ni moja ya vipaumbele vya serikali.

Kiongozi huyo aliwasilisha maombi hayo juzi katika Mkutano wa 10 wa Tume ya Pamoja ya Ushirikiano katika Masuala ya Uchumi, Ufundi na Sayansi kati ya Tanzania na India, uliofanyika kwa njia ya mtandao.

"Ninapendekeza Serikali ya India ianzishe ushirikiano na Tanzania katika kuendeleza sekta ya uchumi wa bluu, hususan uvuvi wa bahari kuu, uendelezaji wa viwanda vya kusindika samaki, utafutaji na uokoaji na utengenezaji wa boti," alisema Balozi Dk. Shelukindo.

Aliitaja India ni mshirika mkubwa na muhimu wa Tanzania katika sekta mbalimbali kama za biashara, uwekezaji, uendelezaji wa miundombinu, ulinzi, elimu na elimu ya ufundi.

Alisema India ni nchi ya tatu kwa kufanya biashara na Tanzania, ambapo takwimu zilipo zinaonyesha kuwa biashara kati ya nchi hizo mbili kwa mwaka 2021/22 ilikuwa na thamani ya Dola za Marekani bilioni sita.

Aliongeza kuwa India ni moja ya nchi tano zinazoongoza kwa uwekezaji nchini kwa kuwa na miradi yenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 3.68, huku takwimu za Kituo cha Uwekezaji Tanzania zikionyesha nchi hiyo kwa mwaka 2021/22 imeandikisha miradi 630 iliyotoa ajira mpya zaidi ya 60,000.

Katibu huyo pia aliishukuruu India kwa kutoa misaada mbalimbali nchini katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na sekta ya maji.

Alisema Tanzania inathamini mchango wa India kwa kutoa mikopo ya masharti nafuu ya Dola za Marekani bilioni moja kwa ajili ya kuendeleza miradi ya maji ambapo mwezi Juni, 2022, kampuni sita zilisaini ujenzi wa miradi ya maji yenye thamani ya Dola milioni 500 kwenye miji 28 itakayofaidisha zaidi ya watu milioni sita, ujenzi wake utakapo kamilika.

Wajumbe wa Mkutano huo ambao walikuwa Makatibu Wakuu wa Wizara, Naibu Makatibu Wakuu au wawakilishi wao walipendekeza maeneo mapya ya ushirikiano na India katika sekta za kilimo, TEHAMA, maji, michezo na utamaduni.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**3 FORM 58**
**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 632 OF 2022**
**In the Matter of the Estate of the Late**
**PRISCA LEONARD NG'ODA**
**and**
**In the Matter of Application for letters of administration by**
**MAKUMBUSHO MWAPOLOLO MWABWAGILO**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above-named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 19 day of July, 2023.

Dated at DAR ES SALAAM this 21 day of June, 2023.

Senior Resident Magistrate

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SEBASTIAN BENEDICT LYANDER** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA CAMI** yenye usajili namba **T935 BMX, CHASSIS NAMBA: J122E007676** na **ENGINE NAMBA: K3EAA7676** .kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **POLISI TAARIFA: DAR/URA/RB/105945/2023**

## KUPOTELEWA NA CHETI



**WEMA FREDRICK OJODE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1590-0025** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MWERA VISION SEKONDARI** mwaka 2012. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **DAR/TAB/RB/219693/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PANGANI EDWARD MBUNGU** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA LITEACE** yenye usajili namb: **T144 DXD, CHASSIS NAMBA: KM850003221 na ENGINE NAMBA: 7K03221**. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: IRI/IRI/RB/221156/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SEBASTIAN BENEDICT LYANDER** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA CAMI** yenye usajili namba **T935 BMX, CHASSIS NAMBA: J122E007676** na **ENGINE NAMBA: K3EAA7676** .kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **POLISI TAARIFA: DAR/URA/RB/105945/2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya MOROGORO**
**Kituo cha CHAMWINO**
**Mkoa wa MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi Na. 14/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU**
**HAMAD SAIDI KIONE wa MOROGORO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA SHAIBU HAMAD KIONE**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe **18** Mwezi **07** mwaka **2023** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia:** Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa

* Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani na waweza kukaguliwa
* Marehemu hakuacha wosia *Futa isiyohusika

Imetolewa leo tarehe 28 mwezi 06 mwaka 2023

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo KIHONDA**
**Wilaya ya MOROGORO**
**Mkoa wa MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi Na. 39/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU**
**HASSAN SAID MWAIPOPO wa MAZIMBU MOROGORO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOTOLEWA NA ASHA HASSAN MWAIPOPO**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 03 Mwezi 07 mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia:** Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa

* Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani na waweza kukaguliwa
* Marehemu hakuacha wosia *Futa isiyohusika

Imetolewa leo tarehe 30 mwezi 06 mwaka 2023

HAKIMU

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA WILAYA YA NYAMAGANA**
**RUFAA YA MIRATHI NO. 07/2023**
**JULIANA MAGESA..........MLETA RUFAA**
**DHIDI YA**
**SINGI MAGESA............. MJIBU RUFAA**

**KUITWA SHAURINI**

SHAURI LA RUFAA LIMEPANGWA KUSIKILIZWA MNAMO TAREHE **05/07/2023 SAA 02:00 ASUBUHI** UNAARIFIWA KUJA KUSIKILIZA SHAURI LILILOFUNGULIWA DHIDI YAKO.

ZINGATIA KWAMBA KUTOKUFIKA KWAKO TAREHE HIYO, SHAURI LITAANZA KUSIKLIZWA BILA WEWE KUTAARIFIWA TENA, NA MAAMUZI KUTOLEWA.

IMETOLEWA KWA MKONO WANGU NA MHURI WA MAHAKAMA HII LEO TAREHE 20/06/2023.

PRINCIPAL RESIDENT MAGISTRATE MWANZA
J.A.Mpuya
HAKIMU MKAZI MKUU
MAHAKAMA YA WILAYA NYAMAGANA
MWANZA

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**Probate and Administration Cause No. 60 of 2023**
**In the matter of the Estate of the late**
**JACKSON MALESA MALINDILA of MKONZE within Dodoma Region**
**And**
**In the matter of the application for letters of administration by ANJELINA MGALAI LÁZARO**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 163)**

All PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 3 Day of JULY, 2023

**Date at Dodoma this 20 day of MAY , 2023.**

RESIDENT MAGISTRATE

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**Probate and Administration Cause No. 64 of 2023**
**In the matter of the Estate of the late**
**IVAN GASPERY MAVIKA of Nkuhungu**
**within Dodoma Region**
**And**
**In the matter of the application for letters of administration by JOSEPHINE JACKSON CHIGWALA AND MARYGOLD MAURILIYO MAVIKA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 163)**

All PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 3 Day of JULY, 2023

**Date at Dodoma this 30 day of MAY, 2023.**

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTELEWA NA VYETI



**NEEMA HUSSEIN** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1153/0043** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **BUSERESERE SECONDARY SCHOOL** mwaka **2013** na cheti cha **CHUO CHA UALIMU** chenye usajili namba **E0628/0091** kilichotolewa na **RICHRICE TTC** mwaka **2016**. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: MWA/NY/RB/202021/2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA YA MBEYA**
**KITUO CHA MWANJELWA MKOA WA MBEYA**
**SHAURI LA MADAI NA.12/2022**
**SABINA NDUNGURU.................MDAI**
**MKURUGENZI W M/S ALOMSHA...MDAIWA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**KWA:MKURUGENZI WA M/S ALOMSHA WA VETA-MBEYA**

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake ya kukazia hukumu,unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 06/07/2023,saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta ushahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

ANGALIZO:Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

**Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa mahakama hii leo tarehe 27/06/2023.**

**HAKIMU MKAZI**
**MAHAKAMA YA MWANZO**
**MWANJELWA**
**MBEYA**


**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 0677020701**
**E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,**
**WEBSITE: WWW.IPPMEDIA.COM**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuzi kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MBWA mmoja wa jirani wa maeneo ya Kinondoni Msisiri, alionekana kuvutiwa na kiroba kilichotupwa upenuni mwa nyumba moja. Ni moja kati ya viroba ambavyo hutupwa usiku au alfajiri na vijana wanaokusanya taka kwenye nyumba za watu na kupewa ujira kidogo. Wao badala ya kwenda kutafuta maeneo ya kutupa, hupita vichochoroni na kama hajaonekana anautupa mzigo na kuendelea na safari yake. Ilitokea kwenye nyumba moja huko, na mbwa huyo alipouvuta, viungo vya mwili wa binadamu viliangukа. Majirani wa kwanza kuona walipiga kelele na watu wakajazana. Akinamama wakiangua vilio. Viungo vilihifadhiwa kwa kufunikwa. Polisi walianza msako. Kwa kuanzia tu wakaanza kuwakamata wazoa taka na waokota chupa za kwenda kuuza, wote wa maeneo hayo na jirani wanaofahamika tayari kwa mahojiano na uchunguzi, wakihisiwa kuwa huenda mmoja wao au zaidi kuhusika na mauaji. Ni maiti ya nani? Na Muuaji ni nani? Fuatilia mwanzo hadi mwisho kujua mkasa mzima ulivyokuwa.

# Maiti kwenye kiroba-15

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Eddy alimuachia kazi hiyo bosi wake na alimpata mmoja ambaye alikuwa amelipwa na matajiri waliokuwa wanataka kumzuia asiende kukomesha tukio moja la wananchi kunyang'anywa ardhi yao na kupewa mwekezaji feki.

Rashid alikuwa amemletea taarifa kuwa yule msafiri aliyepanda ndege kutoka Mwanza kwenda Dar aliwaambia wenzake kwamba anabaki huko kwa sababu alikuwa amepata mpenzi. Na akakodi chumba namba 210 kwenye Hoteli ya Kangaroo.

Na katika uchunguzi kwenye hoteli hiyo ilionekana walilala watu wawili mtu na mpenzi wake na aliondoka kesho yake jioni. Jina la mtu huyo ndiyo lile lile ambalo Eddy analo mkononi. Alitabasamu. Akamsifia jamaa kwa kuwa mtaalam wa kuficha ushahidi.

“Mtu huyu huyu mmoja, alibaki Mwanza wakati wafanyakazi wenzake wanarejea kazini Dodoma baada ya kumaliza semina. Akalala Mwanza kwenye hoteli ya Kangaroo, akiwa na mpenzi wake hadi kesho jioni akaondoka kurejea Dodoma na basi. Lakini mtu huyo huyo ndiye anaambiwa siku hiyo alipanda ndege asubuhi kuja Dar es Salaam na kesho yake jioni akaonekana Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere akielekea Dodoma. Akajikuta akiona kabisa kuwa hachezi na mtu wa kawaida. Japo si kivile, lakini ni mwerevu na mjanja.

Akainua simu na kumpigia Maria.

“Samahani Maria, leo nina kazi nyingi sana, naomba unisaidie kitu kimoja tu.”

“Kipi?”

“Kuna utata kidogo kuhusu hii inshu ya yule jamaa yetu wa Mwanza kuja Dar. Naona fanya kila njia unipatie video ya CCTV kamera siku hiyo anayoshuka kutoka huko, na kesho yake wakati anaondoka.”

“He, mchumba kwani huniamini siku hizi?”

“Hahahahaha, nakuamini, ndiyo maana nilikupa mume, nisingekuamini nisingempa mtu yeyote, matatizo yangu ningebaki nayo, ila ndugu yangu huyu mtu ni mjanja, tarehe hiyo ambayo inaonyesha kashuka huko, kuna taarifa nyingine kuwa alikuwa yupo Mwanza na akalala kwenye hoteli moja mpaka kesho yake asubuhi..”

“Wala haina tatizo Eddy kesho jioni nakutumia, sasa na huko Mwanza umefanya mchakato wa kupata CCTV kamera kama amelala kweli?” Maria akauliza.

Eddy akaangua kicheko.

“Unasikia Maria kwa sababu ninazo




**“Kuna utata kidogo kuhusu hii inshu ya yule jamaa yetu wa Mwanza kuja Dar. Naona fanya kila njia unipatie video ya CCTV kamera siku hiyo anayoshuka kutoka huko, na kesho yake wakati anaondoka.”**

picha za mtu huyo, nikipata video ya CCTV ya hapo tu Uwanja wa Ndege, basi nitakuwa na uhakika kama ni yeye au si yeye. Kama ni yeye basi hawezi tena kuwa siku hiyo hiyo yupo Mwanza. Mtu mmoja hawezi kuishi sehemu mbili kwa siku moja.”

****************************************

Eddy alitabasamu. Mtu mwenyewe ni yule yule. Aliyekuwa kwenye picha aliyoipata na yule aliyemuona kwenye kamera ya CCTV ni huyo. “Kazi nzuri.” Akajiambia mwenyewe. Nadhani pia akamwambia na Maria.

Alimuona mtu huyo alishuka kwenye ndege, akipita kwenye sehemu zote anazotakiwa kupita CCTV ya nje ikampokea na kumuonyesha akienda moja kwa moja hadi kwenye taxi moja inayopaki maeneo hayo hayo ya Uwanja wa Ndege ya Julius Nyerere.

Alichokuwa akikiangalia ni video iliyodurufiwa na Maria kama alivyomuagiza. Maria alimtumia video hiyo kwenye email. Hakutaka kutumia njia nyingine ya mtandao kwa kuhofia kuvuja. Alikuwa ameifungua na kuitazama.

Alibonyesha batani ya kusimamisha. Alisimamisha eneo ambalo namba za taxi hiyo zinaonekana vizuri. Akatwaa kalamu yake na kuziandika kwenye karatasi yake pembeni.

Halafu akabonyeza tena batani ya kuendelea kuitembeza. Aliiangalia tena na tena hadi aliporidhika na kila kitu. “Ni yeye.” Akajiambia.

Sasa kazi iliyobaki kwake ni kuanza kumpeleleza mtu huyo. Na si kumpeleleza kwa kumfuata na kumkamata la hasha. Hakuna ushahidi wowote unaoonyesha kuwa ni ndiye muuaji. Ukimkamata na kumpeleka mahakamani anakushinda mapema tu asubuhi. Hata Eddy mwenyewe mpaka sasa hawezi kuthibitisha. Alichokuwa anakitafuta awali ni majina ya watu mbalimbali aliyoyauliza kimtego kutoka kwa mjomba wa marehemu Tessy. Halafu katika upembuzi yakinifu alivutiwa na kuanza kufuatilia jina la mmoja wapo. Je alikuwepo Dar siku ambayo inadaiwa mauaji yanafanyika? Kilichoonekana ni kwamba hakuwepo. Kwa kujiongeza alimuuliza Maria, mfanyakazi wa Uwanja wa Ndege ambaye alivunja kitendawili kwa kumletea jina la mtu huyo kuwa aliwasili Dar es Salaam na ndege kutoka Mwanza. Kwa nini Mwanza wakati anafanya kazi Dodoma kama alivyoambiwa awali? Ikaonekana alikwenda kwenye semina. Hata hivyo ikaonekana aliwadanganya wenzake kuwa anabaki Mwanza, lakini akapanda ndege kuja Dar. Kwenye hoteli ya Kangaroo kuna mwanaume amelala na demu, akaandika jina la huyu jamaa aliyetoroka kuja Dar.

Kwa hili pekee, Eddy alijua kabisa kuna jambo ambalo si la kawaida. Kama alikuja Dar kwa nia nzuri kwa nini adanganye? Kwanza kwa nini asirudi na wenzake Dodoma halafu akapanda ndege kuja Dar? Kwa nini aliwadanganya wafanyakazi wenzake kuwa anabaki Mwanza? Ni ukweli usiopingika kuwa aliyekuja Dar ndiye yeye na aliyelala Mwanza ni mtu mwingine aliyeamua kuandikisha jina lake. Kwa nini aandikishe jina lake? Eddy aligundua kuwa kulikuwa na nia ovu.

“Huyu si mtu mzuri, inabidi afuatiliwe. Amemtengeneza mtu Mwanza na kumpeleka kwenye hoteli ya Kangaroo, akatumia jina lake ili ionekane yeye alibaki huko, ili hata upelelezi ukifanyika ionekana siku ya mauaji alikuwa Mwanza. Halafu yeye akapanda ndege kuja Dar. Kufanya nini? Na siku aliyokuja ndiyo mjomba wa Tessy anasema mpwa wake hakuonekana.” Akajiambia Eddy.

Kwa asilia nyingi tu, Eddy alianza kuwa na wasiwasi kuwa huyu ndiye muuaji wa Tessy. Atampata vipi? Ushahidi ataupata na kuukusanya vipi ili dunia iamini?

Alichofikiria tangu mwanzo hi hicho hicho kuwa siyo kumpeleleza yeye, ni kuanza kupeleleza nyendo zake siku hiyo alipotua Dar kutoka Mwanza. Alishia kuondoka na Taxi ambalo tayari Eddy alikuwa ameshainakili namba yake.

“Nitaanza kwa dereva taxi huyu, hapa nitaanza sasa kufuata nyayo moja baada ya nyingine za muuaji wa Tessy, ili kujua kama alimuua kwa mkono wake, alitumia watu, kwa nini alimuua kinyama kiasi hicho, na sababu ni nini? Wakati huo wote atakuwa akikusanya ushahidi ili ukipelekwa mahakamani asichomoke. Kazi ya mwisho ni kumtia mbaroni.”

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

HABARI MICHEZO

# KMC KUTUMIA BILIONI MOJA KWENYE USAJILI

**Na Adam Fungamwangwo**

KLABU ya KMC imesema kuwa imepanga kutumia Sh. Bilioni moja kwa ajili ya usajili wa wachezaji kuelekea msimu ujao wa ligi kuu na hawatasajili wachezaji 'makapi'.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Christina Mwagala amesema kiasi hicho kimetengwa kwa ajili ya kusajili wachezaji bora, wenye uwezo mkubwa kwa ajili ya kuifanya klabu hiyo kuwa tishio msimu ujao.

"Tutafanya usajili mkubwa sana, Mkurugenzi wetu Mama Hanifa Selemani Hamza, ametenga kiasi cha Shilingi bilioni moja kwa ajili ya kufanya usajili, na kwa nini ametenga kiasi hicho, ni kwa sababu mikakati yetu ni kuona msimu ujao wa 2023/24 tunakwenda kwenye nchi ya ahadi, maisha magumu tulioyapitia kwa msimu miwili iliyopita haikuwa rafiki kwetu, lazima tufanye usajili wa maana," alisema Mwagala.

Aidha, alisema wachezaji ambao wameshindwa kufanya vyema kwenye klabu zao wasitarajie kuchukuliwa na KMC, kwani hawataki tena wachezaji wa aina hiyo kwa sababu wamewafelisha kwa kiasi kikubwa katika misimu miwi iliyopita.

"Kwa pesa hizi KMC hatusubiri wachezaji makapi, sijui nani kaachwa ndiyo tuende kumsajili, msimu huu hatuchukui wachezaji ambao wameshindwa kufanya vizuri walikotoka, badala yake tutasajiliwachezaji wenye viwango vya juu na wapo tayari kuwavunjia mikataba kwenye klabu zao na kuwasajili," alisema.

KMC kwenye Ligi Kuu msimu ulioisha ilishika nafasi ya 13 baada ya kukusanya pointi 23 na kujikuta ikienda kucheza mchezo wa 'Play Off' dhidi ya Mbeya City kuwania kubaki Ligi Kuu msimu ujao.

Msimu mzuri zaidi ya KMC ulikuwa wa 2018/19 ilipomaliza kwenye nafasi ya nne ya msimamo ikikusanya pointi 55 na ikafanikiwa kucheza Kombe la Shirikisho Afrika.



Brasibendi ya Jeshi la Wananchi (JWTZ) ikitumbuiza wakati wa Mahafali ya 60 ya Elimu ya watu wazima yaliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA.**

# Mpole ataka timu ziongee na FC Lupopo

**Na Adam Fungamwangwo**

MSHAMBULIAJI wa FC Saint Eloi Lupopo ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, George Mpole, amesema kwa sasa klabu yoyote inayomuhitaji inapaswa kufanya mazungumzo na klabu yake hiyo kwa kuwa bado ana mkataba nayo.

Mpole ambaye aliuzwa na klabu yake ya Geita Gold kipindi cha dirisha dogo la usajili mwezi Desemba mwaka jana, alisema alipofika huko alikuta Ligi Kuu nchini humo ikiwa imesimamishwa na Mamlaka za Serikali, hivyo hajawahi kucheza mechi yoyote ya mashindano zaidi ya zile za kirafiki tu.

"Hizi taarifa kuwa kuna timu zimenisajili kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara si za kweli, kwa sababu mimi nina mkataba wa mwaka mmoja na Lupopo, ila kama kweli kuna klabu inanitaka izungumze na viongozi wangu, wavunje mkataba mimi sina wasiwasi kazi yangu ni mpira tu, bahati mbaya sana ni kwamba niliposajiliwa ile kufika tu Congo ligi ikasimama, sijaelewa wala kufuatilia sana sababu ni nini, lakini hadi leo haijachezwa, walikuwa wanacheza michuano ya Kombe la Shirikisho, ilibidi wawe wanatafuta mechi za kirafiki kwa ajili ya kuwaweka fiti tu wachezaji," alisema Mpole.

Aidha, alibainisha kuwa mfumo wa Congo na Tanzania ni tofauti, kwani huko wachezaji hawawekwi kambini kama huku, badala yake unapaswa ujiongoze mwenyewe.

"Kule nimekuta kitu kingine tofauti, wachezaji wanakaa majumbani tu, siyo kama huku, unajiweka fiti mwenyewe kwa sababu mpira ni kazi yako, hawatarajii ukafanya mambo mengine tofauti na ukifanya hivyo namba yako itachukuliwa na unaweza ukapoteza kazi kabisa, kule wachezaji wengi ni wazuri na wanaitaka namba muda wote, na hata kwenye mazoezi ya 'Gym' unajilipia mwenyewe, wanaamini wewe unacheza soka na unalipwa, kwa hiyo utajitunza mwenye siyo kama huku muda wote watu wapo kambini," alisema Mpole.

Kabla ya kuelekea Kongo, Mpole alihusishwa kutakiwa na vigogo wa soka nchini, Simba, Yanga na Azam, kwa sasa anahusishwa kutakiqwa na timu iliyopanda daraja ya Tabora United (zamani Kitayosce).

## Kasongo: Msimu ujao tutakuwa wakali zaidi

**Na Abdallah Mataka**

BODI ya ligi kuu Tanzania Bara (TPLB) imesema msimu ujao wataendelea kuwa wakali kwa klabu zote zitakazovunja sheria na kanuni zilizowekwa.

Alisema kila msimu wanajipanga kusimamia kanuni na hawatamuogopa au kumuhurumia mtu au klabu yoyote itakayoenda kinyume na kanuni hizo.

Akizungumza na Nipashe jana, Kasongo alisema msimu ujao hawataangalia miundombinu pekee bali wataingia mpaka ndani ya klabu kuhakikisha zinaajiri watu wenye sifa ambao watasimamia na kufanya shughuli za klabu kwa weledi ili ziweze kutoka hapo zilipo kwenda kwenye mafanikio zaidi.

Kasongo alisema kuwa msimu ulioisha walijikita zaidi katika kufungia miundombinu ambayo ilikuwa haitoi nafasi kwa timu kucheza mpira vizuri kutokana na ubovu hususani sehemu ya kuchezea (Pitch). "Ni kweli msimu uliopita tumefungia viwanja vingi, lakini msimu ujao tutakuwa wakali zaidi kuliko tulivyokuwa katika msimu uliopita, tumeongeza wigo zaidi wakusimamia, hatutasimamia miundombinu tu, tutaangalia timu za vijana katika klabu, je eneo la utawala lina watu sahihi ambao wanatosha kuwepo katika timu husika", alisema Kasongo.

## KMKM yapambana kupata timu ya wanwake

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

UONGOZI wa mabingwa wa soka Zanzibar, KMKM umesema umeanza mchakato wa kusaka timu yao ya wanawake ili kukidhi kanuni za leseni za vilabu za Shirikisho la Soka Afrika, CAF.

Mwezi uliopita CAF iliwajulisha wanachama wake wote kuhakikisha vilabu vya ligi kuu vinavyoshiriki michuano ya CAF zinakuwa na timu za wanawake ili kupata leseni yakushiriki michuanmo hiyo.

Akizungumza na Nipashe, Katibu wa KMKM, Sheha Mohammed alisema uongozi wa timu hiyo wapo mbioni kuipata timu hiyo ya wanawake ili kukidhi mahitaji ya CAF.

Alisema kwakuwa KMKM ni timu ya taasisi hivyo maamuzi ambayo yataamuliwa na viongozi wa timu hiyo yatapelekwa moja kwa moja kwa uongozi mkuu wa KMKM ili kuona timu hiyo ya wanawake inapatikana.

"Muda wowote kuanzia sasa tutaitangaza timu yetu ya wanawake, tupo kwenye hatua za mwisho kabla ya kuitangaza," alisema Mohammed.

Katika hatua nyingine, Katibu huyo alisema klabu hiyo itaanza maandalizi yake mapema ya kushiriki michuano hiyo ya kimataifa.

## ZISIKUPITE

### JURRIEN TIMBER SAFI
BEKI wa Uholanzi, Jurrien Timber mwenye umri wa miaka 22 anatazamiwa kufanyiwa uchunguzi wa kimatibabu na Arsenal baada ya kukubaliana ada ya awali ya euro milioni 42na Ajax**. (De Telegraaf)**

### TORRES AWANIWA
KLABU ya Aston Villa imekubali mkataba wa pauni milioni 35 kumsajili beki wa Hispania, Pau Torres mwenye umri wa miaka 26 kutoka Villarreal. **(Guardian)**

### RICE NA ARSENAL
KLABU ya West Ham bado inasubiri Arsenal kuwasilisha mpango wa malipo unaokubalika kwa ununuzi wa pauni milioni 105 wa kiungo wa kati wa England, Declan Rice mwenye umri wa miaka 24**. (Sun)**

### CAICEDO ANUKIA CHELSEA
CHELSEA inashinikiza kufikia makubaliano na Brighton kuhusu usajili wa Moises Caicedo, huku kiungo huyo wa kati wa Ecuador mwenye umri wa miaka 21, akiwa tayari amekubali maslahi binafsi. **(Fabrizio Romano)**

### HARNANDEZ KUTUA PSG
MLINZI wa Bayern Munich na Ufaransa, Lucas Hernandez mwenye umri wa miaka 27 yuko mbioni kuhamia Paris St-Germain. **(Fabrizio Romano)**

### VEIGA MBADALA WA MOUNT
KIUNGO wa kati wa Celta Vigo, Gabri Veiga mwenye umri wa miaka 21 ametambuliwa na Chelsea kama mbadala bora wa kiungo wa kati wa England anayekwenda Manchester United, Mason Mount mwenye umri wa miaka 24. **(Standard)**

### TORRES AFIKIRIWA
KLABU ya Aston Villa inafikiria kumnunua kwa mkopo winga wa Barcelona na Hispania, Ferran Torres mwenye umri wa miaka 23 na chaguo la kumnunua la euro milioni 25. **(Mundo Deportivo)**

### LOFTUS-CHEEK SAFI MILAN
KIUNGO wa kati wa zamani wa England, Ruben Loftus-Cheek mwenye umri wa miaka 27 yuko nchini Italia kukamilisha uhamisho wa kudumu kutoka Chelsea kwenda AC Milan. **(Standard)**

### LUKAKU AKATAA
MSHAMBULIAJI wa Chelsea na Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 30, amekataa ofa ya pili kutoka kwa klabu ya Saudi Arabia Al-Hilal - yenye thamani ya pauni milioni 45 kwa mwaka. **(Gazzetta dello Sport)**

### JEBBISON AVUTIWA
KLABU za Juventus, Borussia Dortmund na Bayer Leverkusen zinanavutiwa na mshambuliaji wa Sheffield United, Daniel Jebbison mwenye umri wa miaka 19**. (90min)**

### MARTINEZ ATAKIWA
MANCHESTER United na Chelsea zote zinamtaka mlinda mlango wa Aston Villa kutoka Argentina, Emiliano Martinez mwenye umri wa miaka 30. **(Football Transfers)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MANCHESTER UNITED YAMNASA MOUNT

Imefikia makubaliano na Chelsea ya kulipa pauni milioni 55 na baadae kuongeza..

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United imefikia makubaliano na Chelsea kumsajili, Mason Mount, kwa mujibu wa ESPN.

United italipa pauni milioni 55 za awali na nyongeza nyingine ya pauni milioni 5.

Vyanzo viliiambia ESPN kwamba bonasi kwenda kwa Chelsea “zinategemea sana” mechi na mafanikio ya Mount kule Old Trafford.

Vyanzo vya habari viliongeza kuwa, kwa kuwa Mount yuko likizo kwa sasa, uchunguzi wake wa matibabu unapangwa kufanyika wiki ijayo.

Klabu hizo mbili zimeafikiana baada ya Chelsea kutaka awali pauni milioni 70 kumuuza mchezaji huyo wa kimataifa wa England na United wameshuhudia ofa za pauni milioni 40 na 50 zikikataliwa hapo awali.

Mount mwenye umri wa miaka 24 alitarajiwa kuingia mwaka wa mwisho wa mkataba wake pale Stamford Bridge na mazungumzo kuhusu mkataba mpya yalivurugika.

Yeye atakuwa mchezaji mpya wa kwanza wa kocha Erik ten Hag msimu huu wa joto.

Mount anaondoka Chelsea akiwa amecheza mechi 195 katika klabu yake hiyo ya utotoni.

Alikuwa sehemu ya timu iliyoshinda Ligi ya Mabingwa Ulaya chini ya kocha Thomas Tuchel mwaka 2021.

Mount atakuwa sehemu ya kikosi cha Ten Hag kwa ajili ya ziara ya kujiandaa na msimu mpya nchini Marekani, itakayoanzia New York Julai 20.

Anaweza kucheza mechi yake ya kwanza ya United katika mechi ya kirafiki dhidi ya Leeds United mjini Oslo Julai 12.

## HABARI MICHEZO



# MARTINO: MESSI, BUSQUETS HAWAJAJA MIAMI LIKIZO

**NEW YORK, Marekani**

KOCHA mpya wa Inter Miami, Gerardo "Tata" Martino amesisitiza kwamba yeye na wachezaji wajao waliosajiliwa Lionel Messi na Sergio Busquets hawajenda huko kama "likizo."

Martino alitangazwa kuwa bosi mpya wa Miami Jumatano, ambapo anatazamiwa kuungana tena na Messi na Busquets, ambao awali aliwafundisha Barcelona.

"Tulipozungumza na Leo, jana (juzi) nilizungumza na Sergio, tulizungumza kuhusu kufika ili kuwa na mafanikio, kushindana na kushindana vyema," alisema Martino wakati wa mkutano wake na waandishi wa habari.

"Hii inatokea kwetu hata kwa viwango vya kibinafsi, wakati mwingine watu wanaweza kudhani kuja Marekani ni kama likizo... wanasoka ambao watakuja hapa ni kwa ajili ya kushindana."

Mapema mwezi huu, Messi alitangaza uamuzi wake wa kujiunga na Miami, ambayo ilifuatiwa na habari za wiki jana kwamba kiungo Busquets pia atajiunga na klabu hiyo ya Ligi Kuu ya soka ya Marekani, MLS.

Martino aliwafundisha wachezaji wote wawili wakati wa uongozi wake kule Barcelona kutoka mwaka 2013 hadi 2014, pamoja na Messi katika ngazi ya kimataifa na Argentina kuanzia mwaka 2014 hadi 2016.

Martino ambaye anarejea MLS baada ya kuiongoza Atlanta United katika misimu ya 2017 na 2018, alisema mazungumzo na Miami yalianza kabla ya mikataba ya wachezaji wote wawili.

"Nilianza mazungumzo kabla ya kusajiliwa kwa Messi na Busquets," alisema kocha huyo raia wa Argentina.

Pamoja na kuwasili kwa nyota huyo wa kimataifa na bingwa wa Kombe la Dunia la 2022 kwa MLS, Martino alisema Messi mwenye umri wa miaka 36 anaweza kusaidia zaidi kuhamasisha ukuaji wa soka nchini Marekani.

"Nimesoma kwamba wachezaji wa NFL na NBA wanazungumza juu ya hali hii, ambayo inaonekana kuwa nadra sana," alisema.

"Ninaamini kwamba MLS ina mageuzi ya mara kwa mara na mifano ni wachezaji wa soka wa Marekani ambao wanacheza Ulaya, na katika timu nzuri sana za Ulaya. Tayari kuna mchakato ambao umeanza."

# Jurrien Timber mali ya Arsenal

**LONDON, England**

ARSENAL imefikia makubaliano ya uhamisho wa beki wa Ajax, Jurrien Timber, kwa mujibu wa 90minutes.

Washikabunduki hao tayari wamethibitisha kumsajili Kai Havertz kutoka Chelsea wiki hii kwa dili la thamani ya zaidi ya pauni milioni 65, huku wakiwa wamekubali uhamisho wa rekodi ya England na West Ham kwa Declan Rice ambaye atajiunga nao kwa pauni milioni 105.

Ofa ya ufunguzi ya Arsenal ya euro milioni 35 kwa Timber ilipungukiwa na bei ya Ajax ya ya euro milioni 60.

90minutes inaelewa kuwa ada ambayo imekubaliwa itaifanya Arsenal kulipa euro milioni 42 ya awali, ikiongezwa kwa euro milioni 5 katika nyongeza.

Maslahi binafsi tayari yamekubaliwa na kambi ya Timber na sasa inaweza kufungua njia ya kukamilika kabla ya wikendi.

Inaonekana tumaini kuu la



Timber anayecheza upande wa kulia ni kwamba atacheza sambamba na Oleksandr Zinchenko.

Huku rekodi ya Rice ikiwa tayari kuthibitishwa, dili la Timber litamweka nafasi ya 10 kwenye orodha ya muda wote ya ada ya uhamisho iliyolipwa zaidi ya Arsenal, mbele ya Alexis Sanchez, Shkodran Mustafi na Granit Xhaka, lakini chini ya Mesut Ozil, Gabriel Jesus, Thomas Partey na Alexandre Lacazette.

## Ziyech mambo magumu kwenda Uarabuni

**LONDON, England**

TIMU ya Al-Nassr ya Saudi Arabia inaripotiwa kuwa na shaka juu ya uhamisho wa Hakim Ziyech kutoka Chelsea, kwa mujibu wa Mail Sport.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Morocco ni mmoja wa wachezaji kadhaa ambao wanawaniwa na Klabu za Sau Arabia wakati wanaendelea na harakati zao za kusajili wachezaji kutoka Ulaya.

Chelsea hadi sasa imeshuhudia Edouard Mendy akikamilisha uhamisho wa kwenda Al-Ahli, Kalidou Koulibaly kwenda Al-Hilal, na N'Golo Kante kuondoka kama mchezaji huru na kujiunga na Al-Ittihad, huku Ziyech na Pierre-Emerick Aubameyang nao wakitajwa kuwa njiani.

Mahusiano mazuri ya The Blues hao na wajumbe kutoka kwa Klabu nne zinazomilikiwana Mfuko wa Uwekezaji wa Umma wa Saudia yalivutia uchunguzi fulani kutokana na uwekezaji wa hazina ya utajiri katika Clearlake Capital.

Ziyech amekuwa na shida kwa dakika wakati wa msimu uliopita pale Chelsea, licha ya kuonesha kiwango cha kuvutia akiwa na Morocco kwenye Kombe la Dunia la 2022 nchini Qatar.

Mchezaji huyo mzaliwa wa Uholanzi anaaminika kufanyiwa uchunguzi wa kimatibabu wa klabu hiyo uliobaini matatizo ya goti, jambo ambalo limezua wasiwasi kuhusu kuhamiaa kwa timu hiyo ambayo yupo Cristiano Ronaldo.

Tatizo kama hilo hapo awali lilitambuliwa na Paris Saint-Germain wakati wa kumnunua mchezaji huyo kwa mkopo wakati wa dirisha la Januari.

Uhamisho huo hatimaye haukufaulu kutokana na suala la kiutawala muda mfupi kabla ya tarehe ya mwisho kwa upande wa Chelsea, ambayo ilizidisha kufadhaika kwa Ziyech wakati msimu unamalizika.

Katika mashindano yote, Ziyech alifunga mabao 14 na kusajili asisti 13.



HABARI MICHEZO

# YANGA KUTANGAZA USAJILI WA KUSHTUA

**Na Adam Fungamwango**

UONGOZI wa klabu ya Yanga umewataka wanachama na mashabiki wa timu hiyo kujiandaa kupokea taarifa za usajili wa kushtua ambao utaifanya kuendelea kutamba katika soka la Afrika.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ali Kamwe amesema jana kuwa Juma lijalo, wanachama na mashabiki wa klabu hiyo watapokea taarifa nzuri za usajili na mambo mengine ya maendeleo ya klabu hiyo ambayo yataendelea kutikisa.

"Baada ya kumtangaza kocha mpya Miguel Gamondi, hatua inayofuata ni kwenda kwenye uzinduzi wa jezi ambazo tutazivaa kwa msimu ujao wa mashindano na baada ya hapo ni kuanza kutambulisha majembe mapya ambayo yataitumikia Yanga kwa msimu ujao, hivi ninavyoongea 'thank you' bado hazijaisha tunatembeza kwanza hizo, halafu tunazindua jezi baada ya hapo sasa kazi ya kuleta wachezaji wapya inaanza," alisema Kamwe.

Alisema kuwa wachezaji watakaosajiliwa si tu kwamba watakuja kuitumikia na kuipa Yanga mataji, lakini pia wataiongezea thamani klabu hiyo ambayo ni Mabingwa wa Tanzania Bara na Kombe la FA.

"Wananchi wajiandae kupokea wachezaji wa mpira kwelikweli ambao viongozi wamewaongeza kwa ajili ya kusaka mafanikio ya msimu ujao, kwa hiyo wasiwe na wasiwasi, uongozi wao unafanya kazi kwa weledi mkubwa, wakae wakijua wiki ijayo itakuwa ni ya furaha sana kwao tunakwenda kufanya mambo makubwa sana na nawahakikishia wiki itaanza na moto itamalizika na moto," alisema Kamwe.

Alisema pia wiki ijayo watakwenda kuingia mikataba na makampuni mbalimbali yatayoidhamini klabu hiyo kwa msimu ujao wa mashindano yote.

Klabu hiyo itaanza msimu mpya ikiwa na Kocha mpya baada ya kuachana na aliyekuwa kocha wake, Nasreddine Nabi ambaye hakuongeza mkataba baada ya ule wa mwanzo kumalizika.



Bondia Karim Mandonga akiwasili kwenye banda la Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo alipotembelea banda hilo jana kwenye maonesho ya 47 ya Kimataifa Sabasaba yanayoendelea katika viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere, Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Dodoma Jiji yamwongeza mkataba Medo

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Dodoma Jiji imemwongeza mkataba kocha wake Melis Medo na sasa ataendelea kuwepo mpaka mwishoni mwa msimu ujao.

Kocha huyo alijiunga na klabu hiyo Oktoba mwaka jana kuchukua nafasi ya Mrundi, Masoud Djuma ambaye alitimuliwa kutokana na matokeo mabaya ya timu hiyo.

Taarifa kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema uongozi umeridhika na kazi ya kocha huyo na kuamua kumuongeza mkataba huo.

"Tumemwongeza mkataba Medo kwa sababu alivyokikuta kikosi ni tofauti na alivyokitengeza na kilivyomaliza ligi, kusema kweli sisi kama viongozi tulipambana na yeye mwenyewe aliinua viwango vya baadhi ya wachezaji na kuwarudishia morali wale wote waliokata tamaa, kwa hiyo tumempa nafasi nyingine msimu ujao," alisema mmoja wa viongozi wa klabu hiyo.

Aidha, alisema Kocha huyo tayari amewasilisha ripoti yake ya msimu uliopita na wameanza kuufanyia kazi.

Dodoma Jiji ilimaliza nafasi ya tisa katika msimamo wa ligi kuu msimu uliopita ikiwa imecheza mechi 30 ilishinda michezo 11, ilitoka sare nne na kupoteza kupoteza michezo 15na kumaliza ikiwa na pointi 37.

"Kwa sasa tunaipitia ripoti ya kocha na baada ya hapo tutaanza usajili kwa ajili ya msimu ujao, tunataka kusajili mapema ili tuanze 'pre season' mapema, kwa sababu moja ya vitu vinavyoangusha vilabu vingi ni kuchelewa kuanza maandalizi ya msimu mpya, mipango yetu yote kwa ajili ya msimu ujao tutatoa taarifa rasmi hivi karibuni,"alisema kiongozi huyo.

## Kocha Yanga apangua ratiba

INATOKA UK. 24

kutwaa mataji yote ya ndani kama ilivyo msimu 2022/23 Yanga ilipo twaa makombe matatu ya Ngao ya Jamii, Ligi Kuu Tanzania Bara na Kombe la Shirikisho la Azam Sports.

"Tunamsubiri kocha wetu aje, jukumu lote la usajili liko chini yake na hata maandalizi yetu yapo chini yake," alisema Kamwe.

Alisema katika eneo ambalo wapo makini ni la maboresho ya kikosi na wanaamini Yanga itakuwa bora zaidi ya msimu uliopita ambao walifanikiwa kutinga hatua ya fainali ya kombe la ShirikishoAfrika.

## Simba: Tutamuaga Mkude Simba Day

INATOKA UK. 24

waliruhusiwa wakaja na kuagwa kwa heshima," alisema Ahmed.

Alisema maamuzi ya kuhudhuria tamasha hilo na kupokea heshima yake ipo mikononi mwa mchezaji huyo na uongozi wake mpya.

Mkude ndiye aliyekuwa mchezaji mkongwe zaidi ndani ya klabu ya Simba baada ya kuhudumu kwa kipindi cha miaka 13 akitokea timu ya vijana.

Katika hatua nyingine, Ahmed alisema wanasubiri kalenda mpya ya mashindano ya Shirikisho la soka nchini (TFF) ili kujua lini hasa wataanza maandalizi ya msimu mpya.

"Hatuwezi kusema ni lini tutaingia kambi au kufanya maandalizi ya msimu wa 2023/24 hadi hapo tutakapopata kalenda yaTFF ya msimu ujao, maana unaweza kuingia kambini Julai hii kumbe ligi inaanza Septemba, tunasubiri TFF wakishatoa kalenda yao tu na sisi tunaanza sasa maandalizi yetu na ndio hapo tutajua tunaenda kuweka kambi wapi japo taarifa za awali tutaenda Uturuki," alisema Ahmed.

Pia Ahmed aligusia suala la kiungo wao Sadio Kanoute ambapo alisema nyota huyo bado yupo sana ndani ya kikosi cha timu hiyo baada ya kutoonekana muda mrefu hasa katika michezo ya mwisho ya ligi msimu uliopita.

"Tukumbuke mkataba wa Kanoute umebaki mwaka mmoja na yupo sana Simba, wachezaji ambao wamemaliza mkataba na wako katika mazungumzo ya kumuongeza ni Shomari Kapombe na Mohammed Hussein ambao muda wowote wataongeza na kusalia ndani ya kikosi cha Simba na kucheza Super League " alisema Ahmed.

# Michezo

Jumamosi Julai 1, 2023
Nipashe



**Man United yamnasa Mount** UKURASA 21

# KOCHA WA YANGA SC APANGUA RATIBA MAANDALIZI

## ●●●Aomba kusogezwa mbele tarehe ya kambi, ataka kwanza kupata wasaidizi wake ndipo....

**Na Saada Akida**

KOCHA mpya wa Yanga, Miguel Gamondi amepangua ratiba ya viongozi waliyoiweka kwa ajili ya maandalizi kuelekea kwenye msimu mpya wa ligi kuu na mashindano ya kimataifa.

Awali uongozi huo wa Yanga ulipanga timu ianze maandalizi wiki ijayo kwa kwenda kuweka kambi Tunisi, lakini kocha huyo amesitisha na kusogeza mbele siku ya kuanza kwa kambi hiyo.

Taarifa kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema kocha huyo ameomba kusogezwa mbele kwa kambi hiyo na kuutaka uongozi umsubiri mpaka atakapowasili nchini.

Mmoja wa viongozi wa klabu hiyo aliiambia Nipashe kuwa Gamondi anataka kwanza awe na wasaidizi wake ndipo waende kuweka kambi kujiandaa na msimu ujao.

"Uongozi umekubali mapendekezo yake, sasa tunasubiri aje nchini ndipo tutafahamu lini hasa timu itaanza maandalizi na wapi wataenda kuweka kambi, uongozi tulipanga kwenda Tunisi lakini tunasubiri maamuzi ya kocha, kama atapendekeza sehemu nyingine au huko huko Tunisia," alisema Kiongozi huyo ambaye hakutaka jina lake liandikwe gazetini.

Alisema maamuzi yote ya maandalizi ya msimu mpya wameyaacha mikononi mwa kocha wao huyo mpya aliyechukuliwa kuziba nafasi ya Nasreddine Nabi ambaye hakuongeza mkataba baada ya mkataba wake wa awali kumalizika.

"Kocha ana mapendekezo ya wasaidizi wake, sasa nadhani anataka wapatikane wasaini wote mkataba ndipo sasa maandalizi kwa ajili ya msimu mpya yaanze, uongozi tumekubali tunamsubiri," alisema kiongozi huyo.

Alipotafutwa Msemaji wa Yanga, Ally Kamwe alisema viongozi wamekamilisha mambo mazuri na wanamsubiri kocha wao aje ili maandalizi ya msimu mpya yaanze.

Alisema wanataka kuendeleza makali ya msimu ujao kwa

INAENDELEA UK. 23



Miguel Angel Gamondi

# Simba: Tutamuaga Mkude Simba Day

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa klabu ya Simba umesema utamualika na kumuaga kwa heshima mchezaji wake waliyeachana naye, Jonas Mkude kwenye tamasha la Simba 'Simba Day'.

Siku chache baada ya Simba kutangaza kuachana na Mkude aliyemaliza mkataba wake, Kiungo huyo mkongwe anahusishwa kujiunga na Yanga kwa mkataba wa mwaka mmoja .

Afisa habari wa Yanga, Ally Kamwe alinukuliwa juzi akisema klabu hiyo hawatamruhusu mchezaji ambaye wamemsajili kwenda katika klabu aliyotoka kwa ajili ya kuagwa kwa heshima kauli ambayo ilitafsiriwa kumlenga Mkude waliyemsajili.

Hata hivyo Uongozi wa Simba kupitia kwa Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano, Ahmed Ally alisema watakachokifanya uongozi wa klabu hiyo ni kutoa mualiko kwa mchezaji huyo kama ilivyokuwa kwa wachezaji waliopita ambao waliagwa kwa heshima kwenye tamasha hilo.

Alisema huo utakuwa mualiko kwa mchezaji husika licha ya kuajiriwa na klabu nyingine wao wanachokiangalia nini walichokipanga kuhakikisha wanatimiza lengo lao la kumuaga nyota huyo kwa heshima kubwa.

"Sisi tutamualika Mkude tu , kuhusu mwajiri wake kumruhusu au kutomruhusu hilo juu yao, tutatimiza kile tulichokipanga kwa mchezaji wetu huyo, tamasha letu lililopita tulimualika Maddie Kagere ambaye alikuwa tayari ameshapata timu, Taddeo Lwaga alikuwa amesajiliwa na klabu ya Djibouti na wote

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >